UKURASA WA 3
**BUNGE LAANZA VIKAO, MUSWADA KUONGEZA LIKIZO KINAMAMA WANAOJIFUNGUA NJITI KUJADILIWA**

UKURASA WA 10
**SERIKALI YAPONGEZA NMB BIL. 100/- ZA KUKOPESHA WASAMBAZAJI NISHATI SAFI**



UKURASA WA 3
**ABIRIA WAVUNJA GETI NA KULITUMIA DARAJA KIGONGO-BUSISI KABLA YA KUKAMILIKA UJENZI**

UKURASA WA 7
RIPOTI MAALUM -2
**KINACHOKWAZA UONDOSHAJI TAKA ZA PLASTIKI NI HIKI**


# Nipashe

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumanne Januari 28, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581935
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii


## MKUTANO WA NISHATI

# Tanzania yawakuna vigogo WB, AfDB

• **Waguswa** na umeme vijijini; Zambia yaeleza ilivyonusurika kuingia gizani mwaka 2024, TANESCO ikawanusuru... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Banga yumo nchini kuhudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa Nishati. **PICHA: IKULU**

## Hali yazidi kuwa tete DRC, Ruto aingilia



UKURASA 19

# Tibaijuka: Uamuzi huu wa Trump WHO hatari kwa Afrika, AU ikutane haraka



• **Atoa** tahadhari ARV kuadimika... *Ukurasa 19*

**MICHEZO** **RAMOVIC AMVULIA KOFIA MWENDA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (wa pili kushoto), akijadiliana jambo na Rais na Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina, wakati wa mkutano wa kujadili Nishati kwa Wakuu wa Nchi za Afrika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanzania yawakuna vigogo WB, AfDB

**Na Elizabeth Zaya**

WAKUU wa taasisi za fedha ulimwenguni na Afrika wamesema upo uwezekano wa Bara la Afrika kubadilisha sura ya ukanda huo kupitia sekta ya nishati kwa kuweka nguvu ya pamoja kuunganisha rasilimali zilizopo kuhakikisha zinawafikia wananchi wengi ifikapo mwaka 2030.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye Mkutano wa Nishati wa 'Mission 300' uliowaleta pamoja wakuu wa nchi 24, mawaziri na washiriki wengine zaidi ya 2,600 jijini Dar es Salaam jana, wakuu hao walisema ushirikiano baina ya nchi za Afrika utawezesha ajenda hiyo kufanikiwa.

Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga alisema lengo hilo ni gumu kulifikia lakini linatekelezeka kwa juhudi za pamoja.

"Idadi ya nchi zilizopo hapa si ndogo, kwa umoja wetu tukiweka nguvu za pamoja linatekelezeka," alisema Banga.

Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Dk. Akinumwi Adesina, alipongeza Tanzania kwa kufikisha nishati ya umeme hadi ngazi ya vijiji vipatavyo 12,318, akisema ni mfano wa kuigwa kwa nchi nyingine.

Alisema hatua hiyo ambayo Tanzania imefikia inachangia kuchochea maendeleo na ustawi kwa wananchi vijijini.

"Nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Tanzania,Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha wananchi wa Tanzania kufikiwa na nishati ya umeme katika vijiji vyote, jambo hili linastahili kupongezwa kutokana na umuhimu wa nishati hii katika maendeleo," alisema Dk. Adesina.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuhakikisha nishati hiyo inawafikia waafrika milioni 300 wanaoishi chini ya ukanda wa Jangwa la Sahara na kwamba lengo hilo linakwenda kufanikiwa ili kuifungua Afrika kupitia eneo hilo muhimu.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bo Li alisema shirika hilo liko tayari kufanya kazi na nchi za Afrika ili kusaidia Mission 300 kukamilika huku akiwataka wabia wengine kuunga mkono ajenda hiyo kuhakikisha inafanikiwa.

Mkutano wa Nishati Afrika unafanyika kwa mara ya kwanza jijini Dar es Salaam, Tanzania ukiwakutanisha wakuu wa nchi za Afrika kwa lengo la kuwafikishia nishati ya umeme waafrika milioni 300 ifikapo mwaka 2030.

Majadiliano ya jana yalihusisha mawaziri na wadau wa masuala ya nishati na fedha na leo yatahusisha ngazi ya viongozi wakuu wa nchi za Afrika.

Rais wa Benki ya Asia (AIIB), Jin Liqun aliahidi kuchangia Dola za Marekani bilioni 1.5 kwa ajili kuunga mkono jitihada za upatikanaji umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

Mkutano huo wa wakuu wa nchi wa Afrika ulianza jana na unatarajiwa kufikia tamati leo.

Akifungua mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alisema Tanzania inauchukulia kama kichocheo cha utekelezaji Sera yake ya Taifa ya Nishati inayolenga kuendeleza nishati endelevu, uhifadhi na ufanisi.

Dk. Biteko alisema Tanzania inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati kwa kuwa matarajio yake ni kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda na madini.

Alisema Rais Samia amekuwa mstari wa mbele katika kutafuta suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika, jitihada ambazo zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na kujumuishwa katika azimio litakalotiwa saini katika mkutano huo leo.

Alisema ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025, uzalishaji umeme Tanzania utaongezeka hadi megawati 4,000, kutoka kwenye vyanzo safi.

Alitaja mambo yatakayofanyika katika mkutano huo kuwa ni pamoja na kufungua uwekezaji wa sekta binafsi, kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha mpango wa kufuatilia maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye mkutano huo.

"Ni matarajio yangu kwamba mamlaka zinazohusika za nishati katika kila nchi ya majaribio zitajitahidi kuhakikisha maazimio ya nishati yanafanikishwa kupitia malengo na mipango ya hatua zinazolenga kuongeza kiwango cha upatikanaji umeme, matumizi ya nishati safi ya kupikia, nishati mbadala na mchango wa sekta binafsi katika kufanikisha upatikanaji nishati hiyo," Dk. Biteko alihitimisha.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# ...Zambia yaishukuru Tanzania kipindi kigumu cha umeme

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Fedha na Mipango wa Zambia , Dk. Situmbeko Musokotwane, amesimulia jinsi Tanzania ilivyoivusha nchi yake baada ya kukumbwa na ukame na kupitia kipindi kigumu kwa kukosa umeme.

Akizungumza katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa Nishati unaofanyika jijini Dar es Salaam, Dk. Musokotwane alisema, mwaka jana nchi yake ilikumbwa na ukame mkali na kusababisha uzalishaji wa umeme nchini humo kushuka hadi kufikia asilimia 50.

Baada ya kupitia mkwamo huo, Tanzania ndio iliyosaidia kutatua tatizo hilo kwa kuwapatia nishati ya umeme.

"Tulipata shida hiyo katika kipindi ambacho hatukutarajia na tulikuwa tunajiamini kwa sababu tulikuwa na umeme mwingi wa kutosha tukiuza nje ya nchi yetu, lakini mwaka jana ghafla mambo yakabadilika, tukapata ukame mkali sana na uzalishaji wa umeme ukashuka hadi asilimia 50," alisema Dk. Musokotwane.

"Hali ilikuwa mbaya sana, kwenye sekta ya madini ikawa ni shida, umwagiliaji, na hata sekta ya viwanda kote uzalishaji ukawa ni shida, lakini tunashukuru wenzetu Tanzania ndio walikuja kutusaidia, ninasema asante sana kwa ndugu zangu Tanzania."

Alisema mkutano huo wa nishati umekuja kwa wakati mwafaka na anaamini tatizo la shida ya nishati ya umeme katika nchi hizo linakwenda kutatuliwa.

Alisema jambo kubwa linalohitajika kufanyika kwa nchi hizo kwa sasa ni kuhakikisha wanazalisha umeme mwingi ili kutokwamisha uzalishaji katika sekta nyingine.

"Tunatakiwa tuweke mipango mbadala ambayo itaongeza uzalishaji umeme katika nchi zetu, tutafute vyanzo vingine vya kuzalisha nishati hiyo badala ya kuendelea kutegemea chanzo kimoja na maji," alisema Dk. Musokotwane.

"Kwa mfano Zambia, tuko hapa kwa sababu tuna shida na uwapo wetu hapa unaonesha matarajio yetu kupitia mkutano huu kwa sababu tunatafuta suluhisho."

Aliwaalika wawekezaji kwenda kuwekeza Zambia katika sekta hiyo ya nishati huku akijinadi kwamba tayari nchi hiyo imeweka mazingira mazuri ya kisera katika eneo la uwekezaji.

"Nyie njooni muwekeze, na mkifanya hivyo, mtarudi kuja kushukuru Tanzania kwa kuandaa mkutano huu, maana fursa ziko nyingi na mtakuwa matajiri zaidi," alisema Dk. Musokotwane.

**MAWAZIRI WENGINE**

Waziri wa Fedha wa Nigeria, Adebayo Edun, alisema kama nchi hizo hazitaweka nguvu kubwa katika upatikanaji wa uhakika wa umeme kwa wakati wote, itakuwa ni vigumu kuondokana na umaskini.

Alisema ipo haja kutafuta mbinu mbadala kuondoa tatizo la kukosekana kwa umeme wa uhakika ili nchi hizo zipige hatua kubwa kwenye miradi ya maendeleo.

"Ni lazima tukumbuke kwamba kila sekta inahitaji nishati hii ya umeme, kama hatutawekeza katika eneo hili na kuhakikisha kwamba hakuna tena tatizo la umeme, tusahau kumaliza umaskini katika nchi zetu," alisema Edun.

Aidha, kuna haja ya kufanya mabadiliko makubwa kwenye sera za uwekezaji ili kuruhusu sekta binafsi kuingia na kuwekeza katika sekta hiyo ya nishati ya umeme.

Waziri wa Nishati na Petroli wa Kenya, Opiyo Wandayi, alisema ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa nchi za Afrika kukosa umeme wa uhakika, kuna haja ya kufanya mabadiliko kwa kubuni mbinu mpya hususani za kuimarisha miundombinu ya umeme hasa katika maeneo ya vijijini.

Kadhalika, alisema ipo haja ya kuangalia mbinu nyingine za kuimarisha nishati hiyo ikiwamo ya jua, upepo na jotoardhi na kuharakisha uwekezaji katika nishati jadidifu.

Waziri wa Fedha wa Tanzania, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema Tanzania inahitaji zaidi ya Dola za Marekani bilioni 12.9, kwa ajili ya kuwekeza katika sekta ya uzalishaji wa nishati ili kuwezesha kufikia asilimia 75 ya uzalishaji wa nishati ifikapo mwaka 2030 na asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Alisema lengo ni kufikia asilimia 65 ya nishati mchanganyiko ambayo itawezesha nchi kuzalisha megawati 1,800 za umeme kupitia umeme wa jua, upepo, jotoardhi na maji.

Takwimu za sasa, Waafrika milioni 600 hawajafikiwa na nishati ya umeme.

# Wanging'ombe watenga bajeti ya bilioni 49/-

**Na Elizabeth John,**

WANGING'OMBE

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, limepitisha rasimu ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2025/2026 zaidi ya Sh.bilioni 49.5 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

Akiwasilisha rasimu ya bajeti mbele ya kikao cha baraza la madiwani mwishoni mwa wiki, Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Niceforus Mgaya alisema katika mwaka wa fedha 2025/2026 makusanyo kutoka vyanzo huru ni Sh. bilioni 4.7, mapato lindwa zaidi ya Sh. bilioni 2.3 na zaidi ya Sh. bilioni 42.4 kutoka serikali kuu.

"Katika mwaka wa fedha 2025/2026 halmashauri imekuwa na ongezeko la bajeti ya Sh. bilioni 1.9 ambayo ni sawa na asilimia 4.19 ya bajeti ya mwaka 2024/2025na ongezeko ili limetokana na mapato ya ndani pekee," alisema Mgaya.

Alisema katika rasimu hiyo fedha zaidi ya asilimia 40 zitaelekezwa kwenye utekeleza wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya hiyo ikiwemo ujenzi wa stendi ya mabasi katika Kata ya Wanging'ombe, ujenzi wa kituo cha ukusanyaji mazao Kijiji cha Mambegu.

"Mradi wa kipekee ambao tunakwenda kuanzisha sasa ni maeneo ya utalii, kuongeza kasi ya utalii katika eneo letu ikiwemo Bwawa la Lihogosa ambalo tutaenda kuboresha fukwe na kuleta vifaa ambavyo ambavyo vitatumika kutalii ikiwa pamoja na ununuzi wa boti," alisema Mgaya.

Baadhi ya madiwani, akiwemmo Diwani wa Kata ya Mdandu Anaupendo Gombela alisema mpango wa kujenga standi na vituo vya kukusanyia mazao vitaenda kuchochea uchumi kwa kasi kubwa katika wilaya hiyo.

Awali akizungumza katika kikao hicho Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wangig'ombe, Agnetha Mpangile alisema katika rasimu hiyo kila kata imenufaika na miradi ya maendeleo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe Dk. Peter Nyanja alisema atahakikisha mwaka wa fedha 2025/2026 maboma yote yanakamilika.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zakaria Mwansasu aliitaka halmashauri hiyo kufuatilia mradi wa uchimbaji wa madini ya ulanga kama umeanza rasmi ili uanze kulipiwa mapato badala ya ushuru ambao wanatoa kwa sasa.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha akimwagilia mti baada ya kuupanda, ikiwa ni sehemu ya kusherehekea kumbukumbu ya kuzaliwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika Shule ya Msingi Mapinduzi jana. Jumla ya miti 500 ilipandwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wavunja geti la dharura daraja la J.P Magufuli

**Na Remmy Moka,** MWANZA

ABIRIA na watumiaji wa vyombo vya moto katika eneo la kivuko cha Kigongo-Busisi, mkoani Mwanza wamelazimika kuvunja geti na kupita daraja la dharura linakojengwa daraja kubwa la J.P Magufuli baada ya vivuko kusitisha huduma kwa zaidi ya saa sita.

Kadhia hiyo ilitokea juzi na kusababisha wasafiri wanaokwenda maeneo mbalimbali kukaa kwa muda mrefu wakisubiri huduma hiyo na kulazimu kuvunja na kupita katika daraja hilo.

Akizungumzia adha hiyo kwa niaba ya wasafiri wenzake, John Kipingwa, alisema wamekaa katika kivuko kwa saa tano huku akiiomba serikali kuharakisha jitihada za kumaliza ujenzi wa Daraja la J.P. Magufuli.

Alisema tatizo hilo limekuwa kubwa na la muda mrefu kutokana na wakati mwingine kinabaki kivuko kimoja ambacho hakiwezi kumudu usafirishaji katika eneo hilo lenye shughuli kubwa za usafiri na usafirishaji.

Majid Bashiri, alisema amekuwa katika kivuko hicho kwa zaidi ya saa sita huku akishangazwa na vyombo vyote vya usafiri kuharibika kwa mkupuo jambo linaloleta shida kwa abiria na watumiaji wa vivuko hivyo.

Aidha, alisema baada ya kuuliza waliambiwa kuwa vivuko vyote vimeharibika kutokana na kuingiliwa na magugu maji katika masanduku ya kupozea injini ambayo yalisababisha injini kutofanya kazi kwa ufanisi.

"Tumekaa hapa kwa muda mrefu na mara kadhaa suala hili limekuwa likijirudia, lakini tumeomba kufunguliwa kwa dharura kupita katika daraja la dharura hatujasikilizwa hivyo kulazimika kuvunja na kuvuka kwa mguu kuelekea upande wa pili," alisema Bashiri.

Meneja wa Vivuko Kanda ya Ziwa, Mhandisi Vitalisi Bilauli, alisema tatizo lililojitokeza lilisababishwa na magugu maji ambayo huingia katika masanduku ya kupozea injini.

Alisema hatua hiyo inasababisha kuongezeka kwa joto ambalo halitakiwi na kushambulia injini za vivuko hali inayosababisha kutofanya kazi kwa ufasaha.

"Hadi sasa mafundi wanaendelea na jitihada ili kuhakikisha wanaondoa tatizo hilo ikiwemo kusafisha injini za Vivuko vyote. Mpaka sasa kivuko cha MV. Misungwi tayari kimesafishwa na kinaendelea na usafirishaji hivyo tunaomba wananchi kuwa watulivu," alisema Bilauli.

# Bunge laanza vikao, muswada kuongeza likizo wanaojifungua njiti kuwasilishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO wa 18 wa Bunge unaanza leo vikao vyake jijini Dodoma, huku wabunge wakitarajia kujadili miswada mitano, ukiwamo wa marekebisho ya sheria za kazi.

Miongoni mwa mapendekezo katika muswada huo ni kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa mwajiriwa aliyejifungua mtoto njiti kwa kujumuisha na muda uliobaki kufikia 36 za ujauzito.

Vilevile, muswada huo unapendekeza mwajiri kumpatia mwajiriwa likizo bila malipo isiyozidi siku 30 kutokana na majanga au dharura zinazoweza kujitokeza.

Pamoja na hayo, muswada unapendekeza aina ya mikataba ya muda maalum ili kuongeza wigo wa mazingira ambayo mtu anaweza kuajiriwa kwa mkataba wa kipindi maalum ili kuendana na ongezeko la wingi wa kazi na kutoa fursa kwa wahitimu wa vyuo ili kuwajengea uwezo na kufanya kazi nyingine za misimu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma cha Ofisi ya Bunge, mkutano huo unaanza leo Januari 28 hadi Februari 14 mwaka huu.

Miswada mingine itakayojadiliwa ni ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Tatu na Nne, Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania na Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Mwaka 2024 na tayari ilishasomwa kwa mara ya kwanza kwenye mikutano iliyopita.

Mkutano huo pia utakuwa mahususi kwa kamati za Bunge kuwasilisha taarifa zake za mwaka kuanzia Januari 2024 hadi Januari 2025 na wastani wa maswali ya kawaida 250 yanatarajiwa kuulizwa na wabunge na kutakuwa na maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

## SELCOM MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA, 2024

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 DISEMBA 2024 | Robo Mwaka iliopita 30 SEPTEMBA 2024 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 6,482 | 5,417 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,628 | 14,013 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 110 | 237 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 32 | 22 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 200 | 200 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 66,128 | 63,159 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,357 | 4,775 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,854 | 3,011 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **89,790** | **90,834** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 66,179 | 67,956 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,235 | 1,039 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,579 | 1,610 |
| 27 | Dhima Nyingine | 5,888 | 5,798 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **74,881** | **76,403** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **14,909** | **14,431** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Mchango wa Hisa Uliolipwa | - | 5,000 |
| 33 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (31,371) | (31,371) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,280 | 802 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 37 | Hiza za Upendeleo zilizolipwa | 5,000 | - |
| 38 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **39** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **14,909** | **14,431** |
| 40 | Dhima Zisizo Dhahiri | 429 | 198 |
| 41 | Mikopo Chechefu | 3,276 | 3,157 |
| 42 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 3,389 | 4,254 |
| 43 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16.60% | 15.89% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.71% | 4.68% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 105.04% | 99.20% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 73.65% | 69.53% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 73.87% | 69.75% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -2.61% | -0.76% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1.15% | 5.94% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 31 DISEMBA 2024 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 DISEMBA 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 DISEMBA 2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 DISEMBA 2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 7,289 | 6,657 | 27,941 | 24,916 |
| 2 Gharama za Riba | (1,474) | (1,170) | (5,133) | (4,766) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 5,814 | 5,487 | 22,807 | 20,150 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 498 | (1,493) | (816) | (2,617) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,360** | **1,391** | **5,093** | **5,040** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 118 | 182 | 62 | 174 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 428 | 391 | 1,714 | 1,522 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 814 | 818 | 3,318 | 3,344 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,989)** | **(5,219)** | **(25,287)** | **(20,871)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,546) | (3,105) | (14,099) | (12,426) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (119) | (155) | (548) | (553) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (3,325) | (1,960) | (10,640) | (7,892) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **683** | **166** | **1,797** | **1,703** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (205) | (214) | (517) | (478) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **478** | **(48)** | **1,280** | **1,225** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **478** | **(48)** | **1,280** | **1,225** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 369 | 376 | 369 | 376 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 48 | (5) | 43 | 31 |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.12% | -0.25% | 1.50% | 1.62% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 13.06% | -2.21% | 11.76% | 14.68% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 80.81% | 64.84% | 76.55% | 69.67% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 27.17% | 28.02% | 26.64% | 26.67% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 31 DISEMBA 2024 | Robo Mwaka iliyopita 30 SEPTEMBA 2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 DISEMBA 2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 DISEMBA 2023 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 683 | 436 | 1,797 | 1,703 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 944 | 366 | 2,052 | 4,287 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,969) | (1,654) | (10,888) | (9,898) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (24) | (2) | (35) | (19) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,777) | (521) | 3,944 | 8,806 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 322 | 599 | 1,924 | (1,312) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (369) | 562 | (1,021) | 777 |
| - Kodi Iliyolipwa | (15) | (63) | (204) | (595) |
| - Mengineyo (bainisha) | 192 | (148) | (282) | (465) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(3,012)** | **(425)** | **(2,712)** | **3,285** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (125) | (148) | (437) | (300) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 24 | 2 | 35 | 25 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | - | - | (51) | (669) |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(101)** | **(146)** | **(454)** | **(944)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 5,000 | 5,000 | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (133) | (291) | (952) | (874) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **(133)** | **4,709** | **4,048** | **(874)** |
| | | | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(3,246)** | **4,138** | **882** | **1,467** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **15,872** | **11,734** | **11,744** | **10,277** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **12,627** | **15,872** | **12,627** | **11,744** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa za Kawaida | Mtaji wa Hisa za Upendeleo | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Weka kwa ajili ya hisa | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipindi cha sasa hadi 31 Disemba 2024** | | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2024 | 40,000 | - | - | (31,371) | - | - | - | 8,629 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | 1,280 | - | - | - | 1,280 |
| Hisa za Upendeleo zilizolipwa | - | 5,000 | - | - | - | - | - | 5,000 |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2024** | **40,000** | **5,000** | **-** | **(30,091)** | **-** | **-** | **-** | **14,909** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 31 Disemba 2023** | | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2023 | 40,000 | - | - | (32,537) | - | - | - | 7,463 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | 1,166 | - | - | - | 1,166 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2023** | **40,000** | **-** | **-** | **(31,371)** | **-** | **-** | **-** | **8,629** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2024

| | | |
|---|---|---|
| Imesainiwa na: Julius J Ruwaichi | Afisa Mtendaji Mkuu | Tarehe: 25 Januari 2025 |
| Imesainiwa na: Tajinder Singh | Afisa Mkuu wa Fedha | Tarehe: 25 Januari 2025 |
| Imesainiwa na: Derrick Rushekya | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Tarehe: 25 Januari 2025 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2016, na zinaonyesha hali halisi.

| | | |
|---|---|---|
| Imesainiwa na: Leonard Mususa | Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi | Tarehe: 25 Januari 2025 |
| Imesainiwa na: Tusekile Kibonde | Mkurugenzi | Tarehe: 25 Januari 2025 |

# SELCOM MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|
| **SELCOM RAHISI, NORMAL SAVINGS, RAHISI CAA, ELIMU, AND KIKUNDI ACCOUNT(RAHISI ACCOUNT)** | **TZS** | **USD** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | - |
| Monthly service fees | 2,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | - |
| Bank statement 1free per month | FREE | - |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | - |
| New ATM card issuance | 10,000.00 | - |
| ATM card renewal or replacement | 10,000.00 | - |
| Replacement of the PIN | 10,000.00 | - |
| Standing order Internal | 2,000.00 | - |
| Standing order External | 12,980.00 | - |
| Dormant account fee | FREE | - |
| Interbank Transfer | | - |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | - |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | - |
| >50,000,000 | 10,000.00 | - |
| International transfer | | Up to USD 55 |
| Closure of account | 10,000.00 | - |
| **NUFAIKA TRANSACTIONAL ACCOUNT** | | |
| Required minimum opening balance | 50,000.00 | 25.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | N/A | Up to USD 55 |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **NORMAL CURRENT ACCOUNT (NUFAIKA ACCOUNTS)** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | 0.18% |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | 10 |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement once free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | N/A |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **SPECIAL ACCESS NUFAIKA ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 60,000.00 | 50.00 |
| Minimum monthly turover | 20,000,000.00 | 10,000.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | 0.18% |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement once free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | N/A |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | N/A | 55.00 |
| Dormant account fee | 5,000.00 | 5.00 |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **MIKAKATI SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 20,000.00 | 20.00 |
| Monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 20,000.00 | 20.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | N/A | Up to USD 55 |
| Account closure | 12,000.00 | 5.00 |
| **MIKAKATI PLUS SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | |
| Monthly service fees | FREE | |
| Bank statement once free per month | FREE | |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | |
| Cash withdrawal over counter | ONCE FREE PER MONTH | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 5,000.00 | |
| Dormant account fee | FREE | |
| International transfer | N/A | Up to USD 55 |
| Account closure | 12,000.00 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KIKUNDI SAVING ACCOUNT** | | **TZS** | | |
| Required minimum opening balance | | 10,000.00 | | |
| Monthly service fees | | FREE | | |
| Bank statement once free per month | | FREE | | |
| Bank statement subsequent months | | 10,000.00 | | |
| Cash withdrawal over counter | | 3,000.00 | | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | 3,000 | | |
| Dormant account fee | | FREE | | |
| International transfer | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | FREE | | |
| **BARAKA JUNIOR ACCOUNT** | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | - | - | |
| monthly service fees | | FREE | FREE | |
| Bank statement 1free per month | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cash withdrawal over counter | | FREE | FREE | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | FREE | FREE | |
| Dormant account fee | | FREE | FREE | |
| International transfer | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | FREE | FREE | |
| **TERM DEPOSIT RATES 2024** | | | | |
| **Amount** | | **Interest Rates** | | |
| 5,000,000 - 500,000,000 | | 3% - 12% p.a | | |
| > 500,000,000 | | Negotiation | | |
| **AGENCY BANKING** | **To Govt** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| **Withdrawal (TZS) (agents) Range** | **TZS** | | | |
| 100-2999 | 10 | 450 | 350 | 810 |
| 3000-3999 | 14 | 450 | 350 | 814 |
| 4000-4999 | 27 | 450 | 350 | 827 |
| 5000-6999 | 54 | 450 | 350 | 854 |
| 7000-9999 | 56 | 450 | 350 | 856 |
| 10000-14999 | 102 | 450 | 350 | 902 |
| 15000-19999 | 195 | 450 | 350 | 995 |
| 20000-20000 | 306 | 450 | 350 | 1,106 |
| 20001-29999 | 306 | 1,400 | 700 | 2,406 |
| 30000-39999 | 351 | 1,400 | 700 | 2,451 |
| 40000-49999 | 419 | 1,400 | 700 | 2,519 |
| 50000-99999 | 573 | 1,400 | 700 | 2,673 |
| 100000-100000 | 707 | 1,400 | 700 | 2,807 |
| 100001-199999 | 707 | 2,620 | 980 | 4,307 |
| 200000-200000 | 821 | 2,620 | 980 | 4,421 |
| 200001-299999 | 821 | 3,325 | 1,275 | 5,421 |
| 300000-300000 | 838 | 3,325 | 1,275 | 5,438 |
| 300001-399999 | 838 | 3,950 | 1,650 | 6,438 |
| 400000-499999 | 982 | 3,950 | 1,650 | 6,582 |
| 500000-599999 | 1,245 | 3,950 | 1,650 | 6,845 |
| 600000-699999 | 1,532 | 3,950 | 1,650 | 7,132 |
| 700000-750000 | 1,700 | 3,950 | 1,650 | 7,300 |
| 750001-799999 | 1,700 | 4,850 | 2,250 | 8,800 |
| 800000-899999 | 1,500 | 4,850 | 2,250 | 8,600 |
| 900000-1000000 | 1,776 | 4,850 | 2,250 | 8,876 |
| 1000001-3000000 | 1,875 | 4,850 | 2,250 | 8,975 |
| 3000001-5000000 | 2,000 | 4,850 | 2,250 | 9,100 |
| **Deposit (TZS) (agents) Range** | **To Govt** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| 0 - 20,000,000 | - | - | 100 | - |
| **MOBILE BANKING** | | | | |
| **Withdrawal - Bank to Wallet (TZS)** | **To Govt** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | | | 1,200 |
| 100000.1-300000 | | | | 2,200 |
| 300000.1-500000 | | | | 3,200 |
| 500000.1-1000000 | | | | 4,200 |
| 1000000.1-3000000 | | | | 5,000 |
| 3000000.1-5000000 | | | | 7,500 |
| **Deposit (TZS) (Wallet to Bank)** | **To Govt** | | | **New Customer Fee** |
| 0 - 9,999,999,999 | - | | | - |
| **Air-time top-up** | - | | | - |
| **Utility payments** | - | | | - |
| **Balance inquiry** | - | | | 400 |
| **Mini-statement** | - | | | 500 |
| **Full account statement request** | - | | | 700 |
| **Cheque book request** | - | | | 700 |
| **AMBT internal transfers (same account holder)** | **To Govt** | | | **New Customer Fee** |
| 1 - 5,000,000 | - | FREE | | - |
| **AMBT internal outgoing transfers (other account holder)** | **To Govt** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-750000 | | | | 750 |
| 750000.1-2000000 | | | | 1,000 |
| 2000000.1-5000000 | | | | 1,000 |
| **AMBT External outgoing transfers (Bank to Bank)** | **To Govt** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | | | 3,000 |
| 100000.1-300000 | | | | 3,000 |
| 300000.1-500000 | | | | 3,000 |
| 500000.1-1000000 | | | | 3,000 |
| 1000000.1-3000000 | | | | 3,000 |
| 3000000.1-5000000 | | | | 3,000 |
| **FOREIGN EXCHANGE TRANSACTION** | | **TZS** | **USD** | |
| Telegraphic Transfer - Normal Customer (SWIFT) | | N/A | Up to USD 55 | |
| TISS- Normal Customer | | 10,000.00 | 4.20 | |
| TISS-Staff | | 6,000.00 | 2.10 | |
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | from 3.0% per month to 6.0% per month Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | | from 3.0% per month to 5.0% per month- Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance method. | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | | from 2.5% per month to 6.2% per month - Based on risk Profile/Risk Group of client - on reducing balance method | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | from 2.2% per month to 2.8% per month- Based on risk profile/Risk Group of client.- on reducing balance method | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | 20.40% | N/A | |
| **Loan Processing Fee** | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | 3.70%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | 2.90%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | 1.5% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| **Application Fee** | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | 20,000.00 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | 20,000.00 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | 20,000.00 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | 20,000.00 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | 20,000.00 | N/A | |
| **Insurance Fee Annual** | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | 1.5% | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | 1.5% | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | 2.9% | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | | 1.5% | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | 1.5% | N/A | |

218341802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkutano wa nishati waipaisha Tanzania kimataifa

**TANZANIA** imepata ugeni mkubwa wa zaidi ya marais 25, Mawaziri Wakuu na Manaibu Mawaziri Wakuu, Mawaziri wa Fedha na Nishati 60 wa Afrika, ambao wako nchini kushiriki mkutano wa Nishati wa Mission 300.

Ujio wa ugeni huo ni fahari kubwa kwa Tanzania kwa kuwa pamoja na wageni hao kushiriki mkutano huo muhimu, pia ni fursa ya kipekee ya kutangaza vivutio mbali mbali vya uwekezaji na vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Jiji la Dar es Salaam, ambako mkutano huo unafanyika, limekuwa na shamrashamra za kila aina kuhakikisha wageni wanaoingia wanakutana na mandhari nzuri itakayowavutia kurudi tena.

Miongoni mwa shughuli zitakazofanyika katika mkutano huo ni pamoja na kusaini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika, awamu ya kwanza utakaozishirikisha nchi 14 za Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Pia, utajadili namna ya kutumia fursa ya ushawishi kwa wadau wa maendeleo kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya nishati jadidifu, ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pia imesema baada ya mkutano huo, Rais Samia Suluhu Hassan anatarajia kuwa na mazungumzo na wakuu hao wa nchi kuhusu masuala ya ushirikiano na nafasi ya Tanzania katika kushirikiana na nchi hizo.

Alitaja nchi ambazo wakuu wa nchi wanashiriki katika mkutano huo kuwa ni Algeria, Visiwa vya Comoro, Malawi, Zambia, Sierra Leone, Liberia, Somalia, Lesotho, Botswana, Guinea Bissau, Kenya, Burundi, Mauritania, Congo Brazzaville, Madagascar, DRC Congo, Libya, Khartoum Sudan, Ethiopia, Nigeria, Ghana, Djibout, Togo na Gabon.

Viongozi wengine wanaohudhuria ni Makamu wa Rais wa Gambia, Makamu wa Rais wa Benin, Waziri Mkuu wa Ivory Coast, Waziri Mkuu wa Uganda, Waziri Mkuu wa Visiwa vya Sao Thome, Waziri Mkuu wa Equatorial Guinea, Naibu Waziri Mkuu wa Ufalme wa Eswatini, Naibu Waziri Mkuu wa Namibia.

Kuna mawaziri mbalimbali, manaibu waziri wakuu na Afrika Kusini imewakilishwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati wa nchi, Waziri wa Nishati, Viwanda na Madini wa Tunisia, Waziri wa Mambo ya Nje wa Falme za Kiarabu, Waziri wa Nishati kutoka Rwanda, Waziri wa Nishati Morocco, Waziri wa Nishari Zimbabwe na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Pia, yupo Rais kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika Dk. Akinwumi Adesina na Rais wa Benki ya Dunia, Ajay Banga.


Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) anayeshughulikia masuala ya nishati na mabadiliko ya hali ya hewa, Dk. Kevin Kariuki, amesema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa unakutanisha wakuu wa nchi na viongozi wengine ambao baada ya kujadiliana, watasaini Azimio la Dar es Salaam.

Azimio hilo litaweka makubaliano yaliyofikiwa kutekelezwa kuhusu mkutano huo muhimu na viongozi hao watashuhudia wakikubaliana na kuingia mkataba wa kuwezesha lengo la kusambaza umeme kwa watu milioni 300 kabla ya 2030 kufikiwa.

Ujio wa viongozi hao na ujumbe wao unatoa fursa kwa wafanyabiashara nchini kutangaza bidhaa zao na vile vile, hoteli nyingi zimepata wageni ambao watasaidia kuingiza fedha za kigeni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Joyce Lameck

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hata kama wana usonji tuwapende

**HIVI** karibuni mwimbaji wa nyimbo za Injili Rehema Simfukwe na mumewe Isaya Lyimo, wameikabili dhana potofu kuwa watoto wenye usonji wana tofauti na wengine wenye fahamu na utimilifu wa kimaumbile.

Wamelithibitisha hilo baada ya kumuonesha mtoto wao wa kwanza, Dorcas Lyimo (6), hadharani bila kuwa na hofu wala kudhani watu watasemaje kwa kuwa ana changamoto za kimaumbile.

Hali hii huenda haijawahi kuwa rahisi kwa wazazi wake kuipokea, wamepitia mengi katika malezi ya binti yao huyo ambaye ndiye uzao wao wa kwanza. Pamoja na changamoto zote hawakukata tamaa katika kuhakisha anapatiwa mahitaji muhimu na malezi bora.

Wazazi wake wameielezea jamii historia yake ambayo hatukuifahamu hapo awali, pia wameamua kuanzisha kituo ambacho kitawasaidia wototo wengine wenye tatizo kama la Dorcas, ambacho kimepewa jina la Dorcas Home Care.

Kituo hicho kimezinduliwa rasmi katika maadhimisho ya siku yake ya kuzaliwa ili watoto walio na usonji wanufaike.

Ukweli ni kwamba walio wengi wenye tatizo kama hili wamekuwa wakifichwa ndani na kuwakosesha haki zao za muhimu kama watoto wasio na changamoto.

Pia, wamemuandalia kitabu ambacho kitaelezea historia yake tangu alipozaliwa, hadi sasa ili kueleza jamii yale aliyoyapitia na njia walizochuka wazazi wake na kumfanya kuwa ni mtoto mwenye furaha kama ilivyo kwa wengine.

Naona lipo la kujifunza wazazi wenzangu kutokana na tatizo alilolipata mtoto huyu, kwani kumekuwa na mtazamo hasi kwa jamii pale anapozaliwa mtoto mwenye tatizo la usonji.

Kutokana na imani potofu ndizo zinazowafanya watoto hawa kujiona wana utofauti na wengine, pia kuwa wanyonge kutokana na unyanyapaa wanaupata kutoka kwa baadhi ya watu wa karibu na hata kwa wanafamilia na jamii nzima.

Wazazi, walezi wenye watoto kama Dorcas mnapaswa kuwapenda, kuwajali na kuwapa kila wanachostahili ili kukua na kufanikiwa kwenye maisha yao ili kuwapa furaha na si kujihisi kuwa wana utofauti wakijilinganisha na wengine wasiokuwa na changamoto hiyo.

Ili mzazi uweze kumtambua mtoto wako kama ana usonji, ni vema uwe karibu naye kwa kuzingatia malezi kwani itakurahisishia kutambua kama mtoto ana changamoto hiyo kwakuwa zipo dalili ambazo kama mzazi au mlezi ukiziona utatambua na kumsaidia.

Dalili ya kwanza mtoto kupata shida hiyo ni kushindwa kuwasiliana na kushirikiana na watu , hali inayomuanza tangu udogoni. Anashindwa kuwatizama machoni mama yake, wanafamilia na wengineo wanaomzunguka.

Anafanya mambo yasiyo ya kawaida tena kujirudia, dalili hizi zinaanza katika umri mdogo, mara nyingi wakati mtoto akiwa bado mchanga. Wengine wanaweza kusema hatulii au ni mtukutu hasa anapoanza kutembea na kushika na kuchezea vitu.

Vile vile mtoto anakuwa mzito kuanza kuzungumza au anashindwa kujifunza kuzungumza, anazidi kuogopa kukutanisha macho yake na ya wengine anaposemeshwa na wengine.

Kuna wakati hurudia maneno ambayo watu wengine wamezungumza.

Dalili nyingine ni mtoto kuzungumza kwa mtindo usio wa kawaida, mlezi au mzazi anashindwa kuelewa ikiwa mtoto ana furaha, hasira, au huzuni kutokana na sura yake au lugha ya mwili.

Kwa upande mwingine hupendelea kucheza peke yake kuwa mpweke muda mwingi.

Wazazi wanaihakikishia jamii kuwa usonji unaweza kutibiwa kwa kutumia tiba ya tabia ili kutengeza ujuzi wa kijamii, elimu maalumu shuleni na dawa kama vile vizuizi vya kumwepusha na kujiumiza.

Kuna baadhi ya familia zenye watoto wenye usonji, wanajaribu mlo maalumu au tiba mbadala, japo hakuna ushahidi kwamba njia hizi zinasaidia watoto hao.

Mbali na kuwa na changamoto hiyo wenye usonji wana mchango kwenye jamii, katika mambo mbalimbali kulingana na hali waliyonayo kwani wana uwezo wa kushiriki shughuli mbalimbali.

Wizara ya Afya imeanza kuongeza nguvu katika kuboresha upatikanaji wa huduma za utengamao kwa wenye usonji ikiwemo kuongeza idadi ya wataalamu wa huduma za saikolojiatiba.

La muhimu tusiwabague watoto hawa kutokana na hali zao kwani wote ni sawa kama wengine wenye utimamu kimaumbile na wanahitaji kupendwa, kulindwa na kufundishwa namna ya kumudu na kuendeleza maisha yao.

RIPOTI MAALUMU - 2

# Kinachokwaza uondoshaji taka za plastiki Morogoro hiki hapa

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

***SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana iliangazia namna wakazi wa Manispaa ya Morogoro na maeneo jirani walivyo hatarini kukumbwa na maradhi, ikiwamo saratani, kutokana na kukithiri kwa taka za plastiki zisizorejelezwa.***

***Vilevile, kulikuwa na ushuhuda wa wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ambao walibainisha kuwa wanapomfanyia ng'ombe upasuaji katika hospitali ya mifugo iliyoko chuoni huko, wamekuwa wanatoa tumboni hadi kilo tano za taka za plastiki. Endelea...***



Gari la kubeba taka katika Manispaa ya Morogoro likipeleka taka dampo huku baadhi ya taka zikidondoka barabarani hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

SHERIA ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 {kif 4(1)} inaelekeza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutenga vituo vya kuweka taka kwa muda ambavyo vitatumika kukusanyia taka ngumu kwenye majiji, manispaa, miji au maeneo mengine ambayo yana kiwango kikubwa cha taka ngumu.

Hata hivyo, uongozi wa Manispaa ya Morogoro umekiri kushindwa kutekeleza maelekezo hayo ya kisheria, ukiwa na utetezi "hakuna vifaa na magari ya kutosha kuwezesha uondoshaji taka mitaani".

Sheria inaelekeza eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo, liwe na uzio na lilindwe ili kuzuia wasiohusika kuingia. Lakini kwa kinachoshuhudiwa katika Manispaa ya Morogoro, matakwa hayo ya kisheria yako mbali kufikiwa.

Katika uchunguzi wake, mwandishi wa habari hii amebaini katika maeneo jirani na Uwanja wa Jamhuri, kuna bwaro linaloitwa "Umwema" ambalo linamilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Hilo ndilo limetengwa na manispaa kama kituo cha kuhifadhi taka kabla ya kuzizoa na kuzipeleka kwenye dampo.

Bwaro hili liko katikati ya Mji wa Morogoro. Jirani na eneo hilo la kukusanyia taka, kuna biashara ya chakula. Pia kuna shule mbili za sekondari; Mteule Open School na Chansi, zote zinamilikiwa na watu binafsi na hazina uzio.

Kwenye eneo hilo kumewekwa pipa la kuhifadhi taka ngumu, lakini kutokana na wingi wa taka, pipa hilo limezidiwa, mwandishi akishuhudia wakusanyaji taka kupitia vikundi wakimwaga taka hizo chini na kusababisha mrundikano mkubwa wa taka.

Robert Michael, mkazi wa Manispaa ya Morogoro, anasema taka nyingi zinazopelekwa kwenye pipa hilo, zinatoka kata ya Boma. Anasema kuwa wakati wa mvua taka hizo, zikiwamo za plastiki, zimekuwa zikisombwa na maji na hivyo kuingia mitaroni na baadaye katika mito.

Michael anaelekeza lawama zake kwa uongozi wa Manispaa ya Morogoro, akisisitiza "ndiyo wamepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria za mazingira, lakini kutokuwajibika kwao kunatuweka hatarini kiafya sisi wananchi."

"Eneo hili kama unavyoona kuna shule, wanafunzi wanapita hapa kila siku. Kuna hii njia ambayo watu wa rika zote tunapita hapa na kuna biashara ya vyakula. Mrundikano huu wa taka hauleti picha nzuri kwa jamii," analalamika Michael katika mazungumzo na mwandishi.

Mkazi mwingine wa Manispaa ya Morogoro, Sumai Juma analalamika mrundikano wa taka kwenye eneo hilo unahatarisha afya za wananchi, hasa watoto ambao wamekuwa wakipita eneo hilo kila siku kwenda shuleni, baadhi yao wamekuwa wanaokota chupa za kuchezea kutoka kwenye taka zilizorundikwa.

Albert John, mkazi wa Forest, Manispaa ya Morogoro anasema: "Taka taka zinapokaa kwa muda mrefu pasipo kuondolewa, zinasababisha eneo hili kuwa na harufu mbaya. Tunaomba manispaa ilifunge eneo hili na kutafuta sehemu nyingine kwa ajili ya kuhifadhi taka."

Mkuu wa Kitengo cha Mazingira Manispaa ya Morogoro, Dauson Jeremiah, anakiri mitaa mingi ya manispaa hiyo inakabiliwa na kero ya mrundikano wa taka, akiwa na utetezi "hali hii inasababishwa na uhaba wa magari ya kukusanyia taka".

Jeremiah anasema manispaa inakabiliwa na uhaba wa magari ya kubebea taka kutoka sehemu zilizotengwa kwa ajili ya kuzikusanya na baadaye kuzipeleka dampo la manispaa lililoko Kihonda Mbuyuni.

Anasema Manispaa ya Morogoro ina magari matatu pekee yanayohusika na uzoaji taka na kwamba magari hayo hayakidhi kukusanya taka maeneo yote ya mitaa ya kata zote 59 za manispaa hiyo na hivyo ukusanyaji mkubwa wa taka ufanyike kwenye maeneo machache hasa ya sokoni ambako ndiko kuna uzalishaji mkubwa wa taka.

Jeremiah anasema uhaba wa magari ya kuzolea taka umekuwa unasababisha kero kwa wananchi wa maeneo mbalimbali hasa yenye wakazi wengi kama vile Nanenane, Kihonda, Bigwa na Kilakala.

Anasema kuna vikundi vya usafi ambavyo vimekuwa vinatoa huduma ya kukusanya taka na kuzipeleka kwenye mapipa makubwa ya kuhifadhi taka kwa muda. Mapipa hayo hubebwa kwa magari ambayo humwaga taka hizo kwenye dampo la manispaa.

"Tumeweka mapipa makubwa ya kuhifadhi taka kila kona ya manispaa hii, hasa maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu, lakini changamoto iliyopo ni magari yetu ya kubebea taka. Ni mabovu na ndiyo sababu ya mrundikano wa taka ngumu zikiwamo za plastiki unaolalamikiwa," anasema Jeremiah.

> Wananchi wengi hawana elimu ya mazingira na hivyo wamekuwa nyuma katika kushiriki mikakati ya kukabiliana na taka katika mitaa yao.

Anasema awali kulikuwa na kampuni iliyokuwa inazoa taka katika manispaa yao. Baada ya mkataba kuisha, mmiliki wa kampuni hiyo hakutaka kuendelea na kazi hiyo kwa madai gharama za uendeshaji ni kubwa kulinganisha na faida aliyokuwa anapata.

Kutokana na changamoto hiyo ya uhaba wa magari, Jeremiah anasema Manispaa ya Morogoro inaonekana haifuati kikamilifu maelekezo ya kisheria, akikiri wameshindwa kuwa na uzio katika maeneo ya kukusanyia taka ili kutoruhusu mtu asiyehusika kuingia katika maeneo hayo.

"Sheria ya Mazingira inataka uondoaji taka ufanyike mara kwa mara ili kuepusha kero kwa wananchi na pia kuhakikisha eneo lililotengwa linakuwa na uzio na linalindwa kuzuia wasiohusika kuingia, lakini kwa manispaa yetu ni kweli sheria hii haitekelezwi kikamilifu," anasema.

Jeremiah anafafanua kuwa manispaa hiyo huzalisha tani 377 za taka kwa siku, akitaja maeneo yanayozalisha taka kwa wingi yanajumuisha masoko, biashara ya vyakula na kumbi za starehe.

Ofisa Afya Manispaa ya Morogoro, Ndimile Kilatu anasema Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 inazuia mrundikano wa taka kwa muda mrefu kwa kuwa unaweza kusababisha athari kwa jamii kiafya.

"Maofisa wote waliopewa jukumu la kusimamia usafi wa mazingira, hufanya kazi kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009.

"Mrundikano wa taka karibu na makazi ya watu ni hatari kwani unaweza kusababisha madhara kwa jamii kama vile magonjwa ya mlipuko na hata vifo, hivyo idara zilizopewa jukumu la kusimamia sheria hizo, zinatakiwa kuhakikisha mazingira yanakuwa safi kila siku," Kilatu anasema.

Meya wa Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga, mbali na kukiri manispaa yao kukabiliwa na uhaba wa vifaa vya uondoshaji taka mitaani, anasema kuna kikwazo kingine cha wananchi kutokuwa na elimu kuhusu utunzaji mazingira.

"Wananchi wengi hawana elimu ya mazingira na hivyo wamekuwa nyuma katika kushiriki mikakati ya kukabiliana na taka katika mitaa yao," Meya Kihanga anasema.

Balozi wa Mazingira, Chage Chage anasema kinachoshuhudiwa mjini Morogoro, hasa katika eneo hili la mrundikano wa taka mitaani, ni matokeo ya watendaji wa serikali katika manispaa hiyo kutotekeleza majukumu yao ipasavyo kwenye utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, hata kusababisha mji huo kuwa nyuma kwenye usafi nchini.

***ITAENDELEA KESHO**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF AGRICULTURE

# COTTON DEVELOPMENT TRUST FUND

## JOB OPPORTUNITY ADVERTISEMENT

Cotton Development Trust Fund (CDTF) was incorporated in Tanzania on 4th March 2008 under Trustees Incorporation Act (CAP.318 R.E. 2002) as per certificate of incorporation No. 3352. The Fund is a replacement of the Cotton Development Fund (CDF), which was established under the auspices of the Cotton Industry Act No. 2 of 2001. Formation of the Fund was in line with the wishes of the Cotton Industry Stakeholders as outlined in the Memorandum of Understanding which was signed on 21st April 2006.

Cotton Development Trust Fund is looking for the qualified, young and dynamic Tanzanian to fill in the following vacant position for a Three (3) Months contract.

### POSITION: DRONES OPERATOR (1 POST)

**1.0 Qualifications and Experience Required**

**1.1 Education requirement:**

- A graduate in IT or any engineering related field.
- Must have a valid remote pilot certificate licenced by approved government or recognized authority.
- Good knowledge of agricultural practices particularly in pesticides applications methods and regulations.

**1.2 Experience:**

At least two years' experience and proficiency in agricultural drones operation.

**2.0 Qualitative Requirement:**

- The candidate must have good communication skills
- Should have a good command of English and Kiswahili languages
- Should have good cooperative skills with ability to work effectively with teams.
- Must be 18 years old and above

**3.0 Duties and responsibilities:**

- To teach groups of agricultural officers on best ways to operate drones
- To provide practical and field demonstrations

**4.0 Duty Station: Shinyanga**

**5.0 General Conditions:**

i) Applicants must attach an up to date passport size photo, current Curriculum Vitae (CV) having reliable contact postal address, email address and telephone number(s).

ii) Applicants must attach their detailed relevant certified copies of Academic Certificates as follows:
- Professional certificates
- Form IV and Form VI National Examination Certificates
- Birth Certificate or National Identity Card

(iii) Form IV result slips are strictly not accepted. Presentation of forged academic certificates and other information in the CV will necessitate legal action.

(iv) Applicants should indicate three reputable referees with their reliable contacts in their CV.

(v) Certificates from foreign Universities should be verified by Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Accreditation Council for Technical Education (NACTE) for foreign non degree certificates.

(vi) Only qualified candidates will be contacted for further processes

(vii) Application closing date will be **31st January, 2025.**

**Mode of Application**

Application letters should be posted, e-mailed or hand delivered to the following address:

**DIRECTOR GENERAL,**
**TANZANIA COTTON BOARD,**
**REGIONAL DRIVE ROAD,**
**P.O. BOX 61,**
**MWANZA**

**E-mail: info@tcb.go.tz**

218342902

LINDI JUMBO LIMITED

## INVITATION FOR EXPRESSION OF INTEREST – PRE-QUALIFICATION OF SUPPLIERS FOR BULK SUPPLY AND DELIVERY OF PLANT CONSUMABLES

The Lindi Jumbo Graphite project is situated in southeastern Tanzania, about 200 km away from the port of Mtwara. The project area can be accessed from the southern part via sealed roads that lead from Mtwara to Nanganga, which is approximately 15 km to the north of the town of Ruangwa.

**DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE PRODUCTS:**
Lindi Jumbo Limited is seeking expressions of interest from companies capable of supplying and delivering the following.

| EOI Reference # | S/no. | Item Description | Evaluation Criteria |
|---|---|---|---|
| LJL_2024-102 | 1 | Frother: -Polyethylene Glycol Monobutyl Ether (Butyl-TriGlycol) Mixture, molecular weight approximately 200 g/mol. Dow 200, Flotanol 200, Sasfroth 200, Senfroth 200 or equivalent. Supplied in 1000 IBC. Consumption 1000 kg/month. | 1. Proof of experience in supplying the same products.<br>2. Local content compliance<br>3. OEM, JV or Dealership letter<br>4. Stock capacity and storage in the country.<br>5. Product materials datasheet. |
| | 2 | Flocculant: - Poly acrylamide flocculent, Senfloc 5150, Flopam AN912SH or equivalent. Supplied in 25 kg bags, 40 bags on a pallet. Consumption 1000 kg/month | |
| | | | |
| | 3 | 75 mm rods, 3.8-4m (76.2 Rounds x 3.900M, Grade: SS10/25A) | |
| | 4 | Ceramic Grinding Media (40mm ceramic balls, 3.2 SG) | |
| | 5 | Ceramic Grinding Media (12 mm ceramic beads, 3.2 SG) | |
| | 6 | Ceramic Grinding Media (8 mm ceramic beads, 3.2 SG) | |
| | 7 | Ceramic Grinding Media (6 mm ceramic beads, 3.2 SG) | |
| | 8 | Ceramic Grinding Media (4 mm ceramic beads, 3.2 SG) | |

**Objectives:**

**The primary objectives of The Contractor are as follows:**

1. Timely Delivery: Ensure the punctual supply and delivery of Plant Consumables to Lindi Jumbo's specified location(s) as per the agreed-upon schedule to minimise downtime and disruptions to operations.
2. Quality Assurance: Provide products that meet or exceed the required quality standards and specifications outlined by Lindi Jumbo, ensuring consistency and effectiveness in their application within the mining processes.
3. Reliability and Consistency: Maintain consistent supply capabilities to fulfil Lindi Jumbo's ongoing operational needs, avoiding stockouts or delays in product availability that could impact production schedules.
4. Communication and Transparency: Maintain open and transparent communication channels with Lindi Jumbo's procurement and operational teams, providing regular updates on order status, product availability, and any potential issues or concerns.
5. Compliance: Adhere to all relevant regulatory and compliance requirements, including but not limited to environmental, health, safety, and legal regulations governing the supply and handling of chemical products in Tanzania.
6. Cost-effectiveness: Offer competitive pricing structures and cost-effective solutions while maintaining the quality and reliability of the supplied products and services, optimising overall operational expenditures for Lindi Jumbo.
7. Technical Support: Provide technical support and assistance as needed, including product training, troubleshooting, and on-site support to ensure the effective utilisation of Plant Consumables within Lindi Jumbo's mining processes.
8. Sustainability: Demonstrate a commitment to sustainable practices throughout the supply chain, including environmentally responsible sourcing, packaging, and disposal of products, aligning with Lindi Jumbo's sustainability objectives.
9. Customer Service: Maintain a high level of customer service and responsiveness, addressing any inquiries, concerns, or issues promptly and effectively to ensure a positive and productive business relationship with Lindi Jumbo.
10. Continuous Improvement: Strive for continuous improvement in supply chain efficiency, product quality, and service delivery through feedback mechanisms, performance evaluations, and collaborative problem-solving with Lindi Jumbo's procurement and operational teams.

**PRE-QUALIFICATION REQUIREMENTS**
**COMMERCIAL.**

1. Copy of Company Memorandum and Article of Association
2. Company Profile and Updated Organogram
3. Current Copy of Current Business Licence
4. Recently Copy of Certificate of Incorporation and annual return
5. Tax Clearance Certificate (TCC), TIN Certificate and VAT certificate.
6. Approved Letter for Local Content Plan. Compliance with Mining Act
7. Current audited financial statements 2022/2023, 2023/2024
8. Proof of registration with the Tanzania Revenue Authority (TRA).
9. Capability Statement.
10. Quality Assurance Plan.
11. Material Safety Data Sheets
12. Dealership letter from the OEM or JV with local Tanzanian indigenous company

Companies that possess the ability, capacity, and resources to supply the specified products are invited to express their interest by uploading their proposals via the Procurement portal, www.webportunities.net.
Please note that only proposals submitted via the portal will be evaluated.

All documents must be submitted in English on or before 12:30pm East African Time (EAT) on 15th February 2025. Should you require assistance on the portal, please contact the Tara Nawa team via the portal's Contact Us page.

Lindi Jumbo Limited will review and assess the documents provided by interested companies in accordance with this Expression of Interest (EOI). Evaluations will be conducted based on internal criteria to determine which companies will be included in the list of pre-qualified companies. Only the pre-qualified companies will receive an invitation to bid by signing a Non-Disclosure Agreement (NDA) as part of the call for tender process continuation.

Please be informed that Lindi Jumbo Limited is not bound to accept the lowest or any tender offer received, and the adjudication of the tender will be based solely on the discretion of the company with consideration given to both qualification and commercial aspects.

We look forward to receiving your expression of interest and potentially partnering with your company for the supply and delivery of these essential products.

Lindi Jumbo Limited (Company No. 124563)
Cape Town Fish Market, 3rd floor, Plot No. 180, Msasani Village Block "B" P.O. Box 33773, Dar es Salaam Tanzania
info@lj.co.tz | www.lindijumbo.co.tz

183421



## KANDA KASKAZINI

# Askofu ataka hatua kali kwa watuhumiwa ukatili watoto

**Na Oscar Assenga,** TANGA

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Tanga, Mhashamu Thomas Kiangio ametaka hatua kali zichukuliwe dhidi ya watuhumiwa wa ukatili wa watoto ili kukomesha vitendo hivyo nchini.

Mhashamu Kiangio, alitoa wito huo jana wakati wa ufunguzi wa Jubilei Kuu 2025 kwa waandishi wa habari.

Alisema vyombo vya habari vinatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwafichua watu wanaojihusisha na vitendo hivyo kwa kuleta madhara makubwa kwa watoto na jamii.

"Ukiangalia leo hii watoto wadogo wanahujumiwa, wanaingizwa kwenye mifuko ya rambo, vyombo vipo wapi na je wanatoa taarifa watoto wanatendwa ukatili, wanauwawa wasiokuwa na hatia " alisema.

Alisema wakati mwingine unasikia watoto wamepakiwa kwenye basi kusafirishwa kuelekea mahali fulani, wakiwa hai au wamekufa.

### UKATILI

Akizungumzia kuhusu matukio ya ukatili nchini, Mhashamu Kiangio, alisema Mkoa wa Tanga ni wa pili, hivyo ni wakati wa wanahabari kubadilika kwa kuwafichua wahusika ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua kali.

### DAWA ZA KULEVYA

Askofu Kiangio alisema-Tanga imekumbwa na tatizo la vijana wengine kuingia kwenye dawa za kulevya na kutishia kupoteza nguvu kazi ya Taifa kutokana na kugeuka kuwa tegemezi kwenye familia zao.

"Unapotembea katika maeneo ya Bombo vijana wenye afya na nguvu wameingia kwenye dawa za kulevya wanaenda kupata tiba hapo, serikali inatambua, lakini wale wanaowapa wafikie hivyo ni wakina nani?" Alihoji.

Kiangio alisema inatia uchungu kuona wanaotumia dawa hizo ni ndugu, kaka na dada, hivyo wanahitaji watetezi wa kuwatoa kwenye janga hilo.

Hivyo, alionya kuwa kuna hatari Taifa kuangamia kama hatua hazitachukuliwa kudhibiti matumizi hayo ya dawa za kulevya kwa vijana.

Alisema kinachotakiwa siyo tu kuwaachia wazazi wao kwa maamuzi wanayofanya au ni kuwaachia kupata dawa, bali ni kurudi na kumuomba Mungu kuepusha janga hilo nchini.

### UCHAGUZI MKUU

Akizungumzia kuhusu Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu, Askofu Mhashamu Kiangio, alisema wanafanya jubilee hiyo kumuomba Mungu na kutafakari juu ya Taifa hasa la Tanzania.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi huo wawakilishi na madiwani, wanaomba Mungu awape amani na haki ya binadamu iangaliwe kwanza na watu wawe na umoja na mshikamano katika Taifa.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (wapili kushoto), Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa huo, Peter Toima (watatu kushoto) na viongozi mbalimbali na wanachama wa chama hicho, wakishiriki matembezi ya kuunga mkono maamuzi ya mkutano mkuu wa CCM Taifa ya kumchagua Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea urais mwaka 2025/2030, mjini Babati, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yaimarisha mkonga wa mawasiliano

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imeendelea kujiimarisha kwa mawasiliano katika mpaka wa Tanzania na Kenya wa Horohoro Wilaya ya Mkinga mkoani hapa na kukabiliana na hitilafu na usumbufu kwa wananchi na wafanyabiashara.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa (pichani), alitangaza mpango huo mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kukagua ujenzi wa kituo hicho kutoka eneo hilo kwenda Mombasa nchini Kenya.

"Kwa kuwa na njia hii mbadala ya Mombasa, sasa tunakwenda kuongeza thamani ya bidhaa yetu ya mkongo. Kwa sababu tutaweza kutoa huduma bora na yenye kasi kubwa, bila ya hofu ya kukatika kwa mawasiliano," alisema Silaa.

Alisema hadi sasa mkongo huo, umeunganishwa na nchi za Uganda, Rwanda, Burundi na Malawi na Zambia, huku jitihada zikifanyika kuhakikisha huduma hiyo inafikishwa nchi za Jamhuri ya Demokrasia Congo (DRC) na Msumbiji.

Silaa, alisema lengo la kuongeza mtandao huo wa mawasiliano ni kuhakikisha kunakuwa na njia mbadala ya mawasiliano wakati ya awali inapopata hitilafu.

"Kuimarika kwa mawasiliano ya kimtandao, kutawezesha nchi yetu kukua kiuchumi na wananchi kufikia huduma za kimataifa ikiwemo masoko kwa haraka na uhakika," alisema.

Mkurungenzi wa Ufundi na Uendeshaji wa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Cecil Francis, alisema ujenzi wa kituo hicho umegharimu Sh. milioni 900.

Mkongo huo wa taifa umesogeza huduma za mawasiliano katika wilaya 109 na halmashauri 77 nchini.



# W'biashara wafichua siri vijana kuzeekea nyumba za kupanga

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAFANYABIASHARA mkoani Manyara wameiomba Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi kuhakikisha bei ya vifaa vya ujenzi inadhibitiwa nchini ili kuwapa fursa vijana kujenga nyumba za kisasa na kuepuka kuishi nyumba za kupanga mpaka uzeeni.

Walitoa ombi hilo wakati wakizungumza kwenye kikao cha wadau wa Kodi na tume hiyo kilichofanyika mjini hapa mwishoni mwa wiki iliyopita.

Katibu Mtendaji wa Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti mkoani Manyara (MASUPA), Julian Kambayta, alisema vijana wanashindwa kujenga na kuishi nyumba za kupanga hadi uzeeni kutokana na bei za mabati, saruji, nondo na misimari kuwa ghali.

"Vijana wameniomba niiambie Tume ya Rais ya maboresho ya Kodi kuwa ianzishwe Regulatory Authority ambayo itadhibiti bei za vifaa vya ujenzi," alisema Kambayta.

Alisema wafanyabiashara wa vifaa hivyo, wanatofautiana bei na hivyo kusababisha ugumu kwa wananchi hasa vijana wa kumudu kununua na kuendelea kuishi katika nyumba za kupanga.

Mfanyabiashara, Anna Ulomi, alisema adhabu inayotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) baada ya kuchelewesha kodi iwe na ukomo kwa kuwa inakuwa kubwa kuliko kodi halisi.

"Wapo wafanyabiashara wanapoingia kwenye penali, wengi wanafunga biashara zao maana hazilipiki kabisa," alisema Ulomi

Alitumia fursa hiyo, kuishukru serikali ya awamu ya sita kutodai kodi kwa mtutu wa bunduki na kufunga maduka wakati wakikusanya Kodi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara, Kilimo na wenye Viwanda Tanzania (TCCIA) mkoani Manyara, Musa Msuya, alipendeleza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ilipwe na wafanyabiashara wote badala ya wachache.

"VAT ipungue itoke asilimia 18 mpaka tano," alisema Msuya

Aliishauri serikali inunue mashine za kielekroniki (EFD) na kugawa kwa kila mfanyabiashara anayeanza biashara.

Akitoa maoni yake, Katibu Mtendaji wa TCCIA mkoani humo, Zainab Sadick, alilalamikia utitiri wa kodi na tozo kuwa kero huku bei za mabango ya biashara ni kubwa zaidi ya kutengeneza mabango yenyewe.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Ombeni Sefue, alisema kila wazo, maoni na malalamiko wanayokusanya, yatafanyiwa kazi na kuwasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Mkileta mapendekezo hapa mlete hata kwa maandishi ili tuweze kwenda kuyatetea kwa Rais na takwimu mnazoweka ziwe sahihi maana tunaenda kuzifatilia kujiridhisha," alisema Sefue




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (wapili kushoto) akizindua mikopo maalum ya kuhamasisha nishati safi ya kupikia kutoka Benki ya NMB, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wa (pili kulia) ni Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, (kushoto) ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki hiyo, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yapongeza NMB kwa bil. 100/- za kukopesha wasambazaji nishati safi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepongeza Benki ya NMB kwa kuzindua Mfuko Maalum uliotengewa Sh. bilioni 100 za kukopesha wasambazaji na wauzaji nishati safi ya kupikia kwa watanzania.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, wakati wa uzinduzi wa mfuko huo uliobeba dhamira chanya ya kuunga mkono juhudi za serikali katika Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034).

Kwa niaba ya serikali na Wizara ya Nishati, Dk. Biteko alishukuru NMB kwa wazo hilo, akisema wako tayari kuwaunga mkono ili jambo hilo litimizwe, huku akisema wazo la kuhakikisha mawakala na wasambazaji nishati safi za kupikia wanapata mitaji ili kufikisha huduma mijini na vijijini, litasaidia kuchochea upatikanaji na matumizi ya nishati hiyo.

"Hakika mpango huu wa NMB kutenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya jambo hili unastahili pongezi kubwa sana, hasa ikizingatiwa kuwa kama benki, ina njia nyingi sana za biashara, ambazo wangeweza kuwekeza fedha hizo sehemu nyingine ili kuweza kuendelea kujizalishia faida zaidi.

"Lakini, msukumo huu wa kuja kuweka kiasi hiki kwenye nishati safi ya kupikia inaonesha dhamira ya dhati ya benki kuchangia maendeleo endelevu kwa taifa letu la Tanzania, lakini ni kielelezo tosha cha uzalendo wa kweli uliopo kati yenu menejimenti pamoja na wafanyakazi wa benki hii.

"Mtendaji Mkuu wa NMB tayari ameeleza hapa faida mbalimbali za matumizi ya nishati safi ya kupikia na mimi nisisitize kuwa, faida hizo za afya bora, mazingira safi, kuboresha uchumi na ufanisi wa nishati hizi na ukweli kuwa nishati safi ni salama, ndio maana hata Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa kinara wa hili nchini, Afrika na duniani kote.

Jana na leo, Tanzania ni mwenyeji wa mkutano uliopewa jina la Mission 300 kuakisi dhamira ya kuwafikia watu milioni 300 barani Afrika kuhakikisha wanatumia nishati safi, ambapo marais 25, Mawaziri wa Fedha na Nishati 60 wa Afrika, watashiriki mkutano huo, mwenyeji akiwa Rais Samia.

Kwa kutambua umuhimu wa mkutano huo na kuunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, NMB inaamini kiasi ilichotenga kwa ajili kukopesha wadau wa biashara ya nishati safi, utakuwa na mchango chanya kwa taifa katika azma yake ya kukuza kiwango cha matumizi ya nishati hiyo mjini na vijijini.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema msukumo wa benki yake kutenga kiasi hicho kikubwa cha fedha za kukopesha wafanyabiashara na wasambazaji nishati, unalenga kuwezesha utunzaji mazingira, kuboresha afya na ustawi wa jamii, kukuza uchumi na kuchangia kufikiwa kwa Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Zaipuna alisema lengo ni kuongeza urahisi katika upatikanaji nishati safi kwa watanzania na kwamba NMB inatambua umuhimu wa kuungana na serikali kufanikisha Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi wenye lengo la kuhakikisha upatikanaji nishati nafuu, kwa urahisi, endelevu na ya kisasa kwa wote.

"Takwimu zilizotolewa wakati wa Mkutano wa Clean Cooking uliofanyika jijini Paris, Ufaransa Mei, 2024, zinaonesha kwa nini wadau wote tunapaswa kushirikiana na serikali na wananchi kukabiliana kwa haraka na suala la ukosefu wa upatikanaji nishati safi ya kupikia barani Afrika.

"Takwimu hizo, ambazo ni za kushtusha, zinaonesha zaidi ya watu bilioni 1.2 barani Afrika hawatumii nishati safi za kupikia, na kuwalazimu kutegemea mkaa na kuni kwa kupikia, hali inayochangia madhara makubwa ya kiafya, kimazingira na kijamii na waathirika wakuu wa changamoto hii ni wanawake, ambao ni dada zetu na mama zetu, hasa wa vijijini.

"Matokeo yake, Afrika inapoteza zaidi ya wanawake na watoto 600,000 kila mwaka kutokana na athari za moshi wa utokanao na nishati chafu na Tanzania, kama ilivyoanishwa na Ofisa Nishati Mkuu kutoka Wizara ya Nishati, Mussa Abbas, zaidi wa watu 33,000 hufariki dunia nchini kila mwaka kwa kutokana na athari za nishati chafu," alisema Zaipuna.

Alisema kiwango cha mwisho kwa mkopaji mmoja ni Sh. bilioni moja na mkopo utakuwa wa riba nafuu na rafiki ya asilimia moja kwa mwezi (sawa na asilimia 12 kwa mwaka) na kuwa walengwa wakuu wa mkopo huo utakaopatikana kwenye matawi yote, ni wasambazaji na mawakala wa mitungi na majiko ya gesi ambayo kwa sasa ndio nishati safi zaidi inayopatikana kwa urahisi.

Akimkaribisha Naibu Waziri Mkuu kuzungumza katika uzinduzi huo, Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, alipongeza NMB kuunga mkono juhudi za serikali kufanikisha malenpo endelevu ya kufikisha huduma ya nishati kote nchini na kwamba benki hiyo imefanya jitihada kubwa katika kuwapambania watanzania, wakiwamo wafanyabiashara na wajasiriamali wanawake.

## Mazao kupigwa mnada kwa TV

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) imesisitiza mazao ya wakulima yatauzwa kulingana na mfumo wa biashara wa minada ya kidijitali na stakabadhi ghalani kwa uwazi na haki kwa njia ya televisheni ili kuinua maisha yao.

Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Irene Mlola alisema hayo wakati akiwasilisha mwongozo wa biashara ya mazao ya ufuta, choroko, mbaazi, dengu na soya kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha katika kikao cha wadau wa mazao hayo mkoani hapa.

Irene alisema katika kikao hicho kilichofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita kuwa mkulima atakapouza mazao yake kwa kufuata mifumo hiyo iliyowekwa na Serikali, atakuwa huru kufuatilia akiwa katika kituo maalum au ghala kupitia televisheni na kushuhudia wanunuzi wakishindana kununua mzigo wake.

Alisema uwazi huo utampa mkulima mkusanyaji mazao, fursa ya kuuza mazao yake kwa bei ya maslahi na endapo bei haitakuwa ya maslahi, mtunza mali anaweza kuamuru kusitisha kuuza mazao kusubiri bei itakayompa faida.

"Wakulima tumieni fursa ya kuuza mazao inayotolewa na serikali ni ya wazi na itawasaidia kupata faida kubwa kwa sababu inafanywa kwa uwazi," alisema Irene.

Alisisitiza vipimo rasmi vinavyotambuliwa na wakala wa vipimo nchini, vitatumika kupima mali ya wakulima ili biashara ifanyike kwa haki na hakutakuwa na nafasi ya kufanyika udanganyifu na dhuluma kwa wakulima.

Kwa upande wake, Macha aliahidi serikali ya mkoa huo kushirikiana na COPRA na taasisi zinazosimamia mwongozo wa biashara ili kumnufaisha mkulima.

Alisema kikao cha pamoja na wadau wa mazao hayo mkoani hapa, kitatoa muelekeo wa mikakati ya kufanya kuhakikisha wakulima wananufaika na bei za ununuzi kwa njia ya minada ya kidijitali.

"Nawashukuru sana COPRA kwa kuja Shinyanga kufanya kikao pamoja na serikali ya mkoa. Nawahakikishia wakulima wa mazao hayo watarajie mambo makubwa kwenye ununuzi na uuzaji wa mazao kwa njia ya minada," alisema.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi watendaji wa halmashauri za mkoa huo kushirikiana na COPRA, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kuhakikisha biashara ya mazao hayo inafanyika kwa mafanikio kwenye maeneo yao kwa kufuata mwongozo.

Alisema lengo la serikali ni kuona wakulima wananufaika na kilimo cha mazao yanayolimwa kwenye maeneo yao na kukusanya kodi kwa kutoza ushuru.

Nipashe
TESA
Jumanne Januari 28, 2025
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

UKIWA HAPA UTAPOFUKA

**Stendi, gereji, foleni barabarani, ndani ya lori**



Ukurasa 12

UNENE KUPINDUKIA:

Binzari yaweza kuwa jibu si mazoezi au kuacha kula wanga



Ukurasa 13

Bokotimiza shule inayojinasua kutoka mkiani, sasa ikikaribia kufika 10 bora

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Utoro huu shuleni unavuruga malengo ya Dira ya 2050

TANZANIA 2050, inajinasibu kwenye dira yake ya maendeleo, miaka 25 kuanzia leo inatarajiwa kuwa nchi yenye mfumo bora wa elimu katika ngazi zote.

Dira 2050 inasema mfumo huo utajenga maarifa na stadi za wahitimu tena utashabihiana kwa karibu na sekta za uzalishaji ili kuwapatia ajira au kuwawezesha kujiajiri wanafunzi wake.

Inapoanza kuelekea kwenye hatua hiyo nchi ina sera ya serikali kugharamia elimu kuanzia msingi hadi sekondari, lakini kwa uzembe huu wa wazazi na walezi wanaelekea kuikwamisha dira.

Kwa lugha nyingine ni sawa na kusema licha ya serikali kugharamia elimu, kupuuza na kutojali umuhimu wa taaluma ni tatizo.

Mathalani, utoro wa wanaoanza kidato cha kwanza mwaka huu katika baadhi ya maeneo ni kama mfupa ulioshindikana.

Mfano mmojawapo ni huu wa wanafunzi 5,080 kati ya 6,313 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu katika sekondari za Halmashauri Wilaya Tarime Vijijini mkoani Mara, hawajaripoti shuleni tangu zilipofunguliwa Januari 13, 2025.

Taarifa hiyo inatolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Simion Langoi, katika kikao cha Baraza la Madiwani, wakati wakijadili na kupitisha bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, wiki iliyopita.

Kaimu mkurugenzi anawaomba madiwani wasaidie kwa kuwa wanafunzi wanaishi maeneo mbalimbali ambayo madiwani hao wapo, na kwamba utoro huo ni aibu kwa halmashauri yao na hata taifa.



Uvuvi ni shughuli zinazowavutia wanafunzi na kusababisha utoro katika mikoa yenye mito au bahari ama maziwa. **PICHA :MTANDAO**

Kinachoelezwa na uongozi huo ni mfano mmojawapo kwa mwaka huu wa 2025. Inawezekana kuna maeneo mengine hali ikawa mbaya kuliko sekondari za Tarime Vijijini.

Kama ndiyo Tanzania inayotaka angalau ikifika mwaka 2050 watoto wawe wamesoma na kufikia elimu ya sekondari, kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, itawezekana?

Hao ni wanafunzi wa shule za sekondari moja lakini bado hawajatazamwa wa shule za msingi ambao nao wameanza kusoma mwanzoni mwa mwaka. Ikumbukwe tena ni halmashauri moja na cha kujiuliza hali ikoje kwa Tanzania nzima?

Ni suala la kuwafikirisha si madiwani na watendaji wa vijijini, kata, mitaa na vitongoji hata upande wa kutunga sheria nao ni muhimu ufanye jambo ili kukomesha mtindo huo unaokwamisha maendeleo ya elimu.

Kwa kawaida wanafunzi wanatakiwa kuwahi shuleni baada ya mwaka wa masomo kuanza, lakini baadhi yao kama ilivyo Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Vijijini imekuwa ni tofauti kwani wapo ambao shule inapofunguliwa hawaripoti hadi watafutwe. Inakuwaje mzazi au mlezi?

Imekuwa ni kama mtindo unaoelekea kuzoeleka miongoni mwa jamii kutokana na wanafunzi wachache wa sekondari kuripoti katika shule walizopangiwa huku wengine wakiwa hawajulikani waliko.

Kuna uwezekano baadhi yao wamekwenda katika shule nyingine, lakini ni vyema kuwepo utaratibu wa kueleza mamlaka zinazohusika ili ifahamike. Isionekane kama ni kupuuza masuala ya elimu.

Hata kama watakuwa wamehamia katika shule nyingine, lakini idadi ya watoro wa Tarime Vijijini ni kubwa mno. Kwa idadi hiyo kubwa, ni wazi huenda wapo walioolewa au kubaki wakifanya kazi za nyumbani.

Lakini wanaohama ni vyema wawe na barua za watendaji wa vijiji au mitaa ili kuweka rekodi za ufuatiliaji watoro, kwani utoro una athari nyingi ikiwamo kupungua kwa ufaulu, kuongezeka kwa idadi ya raia wasiojua kusoma wala kuandika mbumbumbu hasa ukianzia darasa la kwanza, kuwa na taifa la wasiohitimu na wasio na vyeti hasa ambao wanaacha shule na hivyo kuathiri maendeleo ya elimu kwa ujumla.

Ikumbukwe kuwa utoro wa wanafunzi hasa wa kidato cha kwanza kila mwaka wa masomo, umekuwa kama jambo la kawaida au ndilo fupa lililoshindikana kutafunwa na fisi na kuachwa libaki kama lilivyo.

Serikali imekuwa ikifanya msako dhidi ya watoro kila shule zinapofunguliwa, ikihusisha kukamata wazazi na walezi, hata hivyo pamoja na juhudi hizo, hali ni ile ile.

Inaumiza kuona serikali ikipoteza rasilimali hasa kujenga majengo au miundombinu, kuweka watendaji na vitendea kazi lakini inaonekana kama jambo la kawaida hata wanafunzi wasioripoti shuleni na nafasi zao kubaki wazi bila sababu ya msingi bila maelezo.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

UNENE KUPINDUKIA

# Binzari yaweza kuwa jibu si lazima mazoezi wala kuacha kula wanga

MARA kadhaa watu wanaambiwa waache ulaji vyakula vyenye wanga mwingi, kuepuka maisha bwete ya kukaa bila mazoezi, kufanya mazoezi, kuachana na sukari,mafuta pia kunywa maji mengi ili kupunguza uzito na mafuta mwilini.

Yote hayo sasa , yanaweza kuwa si jambo la kuwahofisha watu. Ni baada ya Dk. Julian Ross, mtafiti mkuu katika Taasisi ya Tiba ya Johns Hopkins ya Marekani kuyabatilisha.

Ross mtaalamu wa afya mbobezi, anasema yote haya ni nusu kweli, hayajathibitika.

"Njia za kupoteza uzito ambazo watu wengi hutumia na zinazoonekana kwenye mitandao kudhibiti uzito, lakini si kwa haraka au kwa kudumu. Kwa sababu hazishughulikii sababu au chanzo cha tatizo."

Mwishoni mwa wiki Dk. Julian anawataka watu kula wanga kama kawaida. Anasema hivyo kwanini?

Anaeleza kuwa amegundua ujanja wenye mafanikio makubwa na kwamba una nguvu nao ni kutumia binzari ya njano au 'tumeriki'.

Binzari ni jamii ya mimea kama ilivyo tangawizi isipokuwa ina rangi ya karoti , kama ilivyo tangawizi unaweza kuikausha na kutumia unga wake kwenye chakula.

"Ni rahisi. Nimeigundua ni rahisi kwa kutumia manjano, asilimia 100 ambayo yeyote anaweza kutengeneza nyumbani kwa "kula" au kumaliza mafuta yote tumboni."

"Maelfu ya watu ambao wamejaribu njia hii ya kujitengenezea nyumbani na manjano wanasema kuwa wamepunguza uzito haraka katika wiki mbili za kwanza, na kugundua kuwa wapengua kwa kasi kwa kula pipi na vyakula wanavyopenda na bila kwenda kwenye mazoezi au lishe ya aina yoyote."

Wafuasi wa Dk. Julian wameipa mbinu hii jina la utani "Turmeric Hack," kwa sababu ni suluhisho jepesi ambalo hurekebisha tatizo la uzito chapchap kwa kuchoma mafuta ya mwili kikamilifu.



BINZARI YA NJANO TIBA UNENE KUPINDUKIA

Binzari inatajwa kuwa silaha ya kuondoa mafuta na kumaliza viriba tumbo. **PICHA: MTANDAO**



**UZITO UNATISHA**

Wataalam wanasema ukiwa na uzito kupita kiasi au unene unaopitiliza ni chanzo cha kupata matatizo mengi kiafya kama maradhi ya moyo kwa sababu uzito wa ziada hufanya moyo wako kufanya kazi kwa bidii kusukuma damu, ambayo inaweza kusababisha shinikizo la damu na ugonjwa wa moyo.

Kiharusi, ikimbukwe shinikizo la juu la damu linaweza kusababisha kiharusi, ambacho hutokea wakati damu inakwama kuingia kwenye ubongo.

Ugonjwa wa kisukari, aidha kunenepa kupita kiasi ni sababu ya hatari kwa ugonjwa wa kisukari cha aina ya pili kinachopatikana ukubwani. Saratani, inatajwa kwa maelezo kuwa unene huongeza hatari ya kupata aina kadhaa za saratani, ikiwa ni pamoja na saratani ya matiti, koloni na endometriamu au kizazi.

Kukosa usingizi kunaweza kuletwa na uzito wa ziada kwenye shingo unaosababisha ikawa vigumu kupumua usiku na kusababisha kukosa usingizi.

Shinikizo la damu nalo ni zao la uzito wa ziada unaoweza kusababisha mishipa kuwa migumu na kiharusi.

Kadhalika maumivu ya viungo na misuli au maradhi ya ' osteoarthritis', ambayo husababisha maumivu na ugumu katika viungo vya mwili wa mtu mnene.

Ugonjwa wa ini, unaweza kuchochewa na uzito unaosababisha mafuta kujilimbikiza karibu na ini kisha kuharibu tishu ini na kusababisha kovu, na hata ini kushindwa kazi.

Mawe ya nyongo pia yanaweza kutokana na kunenepa kupita kiasi, ambayo hutokea wakati nyongo inapojikusanya na kuwa ngumu kwenye kifuko cha nyongo.

**KUITUMIA**

Poda ya manjano inaweza kutumika kupunguza uzito kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwekwa kwenye chai, maziwa na vinywaji vingine binzari ina hiliki, inayosaidia kupunguza uzito kwa kuongeza 'metaboliki' au shughuli za mwili zinazotumia chakula kingi lakini ikipunguza hamu ya kula. Wataalam hao wanashauri kuchemsha maji na kuweka kijiko cha chai cha manjano au binzari inayochemka kwa takriban dakika tano.

Unaweza kuchuja ukitaka, na ili kupata ladha zaidi unaweza kuongeza chai, juisi ya limao au chochote kuanzia mchaichai na ukishauriwa kuinywa wakati hujala chochote ili ifanye kazi kikamilifu.

Aidha, unaweza kuchanganya maziwa na manjano au binzari hiyo, si mbaya kama una asali unashauriwa kunywa kabla ya kulala.

Unaweza pia kuongeza 'turmeric' au binzari kwenye chakula kama wali, kachumbari, mboga, supu, kwenye kitoweo au kunyunyiza kwenye karanga na vitafunwa vingine.

Manjano yana kichocheo cha 'curcumin,' ambayo inachochea mwili kuchoma kalori kwa ufanisi zaidi. Joto la chai linaweza pia kukata mfumo wa utumbo na kupunguza hamu na tamaa ya kupenda kula zaidi.

Kwa mujibu wataalamu hao ni salama inapotumiwa kwa muda mfupi au mrefu haina athari mwilini. Hata hivyo, inaweza kuchukua miezi kadhaa kuona matokeo makubwa ya kiafya.

# UTORO HUU SHULENI UNAVURUGA MALENGO YA DIRA YA 2050

**INATOKA UK.11**

Ni muhimu sasa kuangalia upya wapi tatizo lilipo na kuleta ufumbuzi wa kudumu kuliko kuendelea kuwa na hali kama hiyo. Kwani utoro wa wanafunzi shuleni unahitaji kushughulikiwa kwa dhati katika zama hizi za utawala, uongozi bora na uwajibikaji kwa maendeleo ya taifa, kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo linalojirudia kila mwaka bila kujua kuwa linaathiri dira na maendeleo ya taifa.

Changamoto hiyo inaweza kushughulikiwa kwa njia ya uwajibikaji na utawala bora kuanzia ngazi ya serikali za mtaa ili kuhakikisha kuwa tatizo hilo linapungua au kumalizika.

Kimsingi, wanafunzi wanaishi katika maeneo mbalimbali ambayo yako chini ya uongozi wa serikali za mitaa. Hivyo, viongozi wa mitaa husika wanapaswa kujua idadi ya wanafunzi waliofaulu na kuwafuatilia.

Kukiwa na mfumo wa kuwafuatilia kuanzia vijijini, vitongojini na serikali za mitaa tangu wanapohitimu na kutangazwa kuingia sekondari, itakuwa rahisi kujua idadi ya wanaohamishiwa shule nyingine na watoro ili wachukuliwe hatua ili kuepusha nchi kukosa uwezo wa ushindani katika nyanya ya elimu.

Ukweli ni kwamba zipo sababisha pia za nchi kukosa uwezo wa ushindani kwenye nyanya za elimu na teknolojia kwa kuwa wengi hawajasoma, si waelewa wa mambo wala si watafuta maarifa.

Baadhi ya sababu zinazochangia ambazo hutwaja kuchangia utoro kwa baadhi ya wanafunzi shuleni ni umaskini, jamii kutojua umuhimu wa elimu, ndoa za utotoni, kutumikishwa watoto kwenye kazi mashambani, ufugaji na uvuvi, kulelewa na wazee bibi na babu wasio na uwezo wa kufutilia mienendo ya wajukuu wao.

Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya mwaka 2022, inaonyesha kuwa mikoa inayoongoza kwa mimba za utotoni na asilimia zake kwenye mabano ni Songwe (45), Ruvuma (37), Katavi (34), Mara (31) na Rukwa (30).

Mara ni mkoa kinara ukiwa kwenye tano bora, hivyo si suala la kufumbiwa macho. Utatuzi wa wake uanze kushughulikiwa kwa njia ya uwajibikaji, viongozi wa serikali za mitaa walisimamie kwa nguvu zao zote ili lipungue au kumalizika.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Bokotimiza shule inayojinasua kutoka mkiani, sasa ikikaribia kufika 10 bora



Wanafunzi wakifurahia jambo shuleni **PICHA: MTANDAO**

SHULE ya Msingi Bokotimiza kwa muda mrefu imeburuza mkia ikishika nafasi ya mwisho kwenye shule za Halamashauri ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani kwenye matokeo ya mitihani ya kitaifa.

Sasa imeondoka kwenye ufaulu wa daraja la C na sasa inaelekea kufikia nafasi ya shule 10 bora za halmashauri hiyo.

Chanzo ni utoro na mwamko mdogo wa wanafunzi, kukosekana ushirikiano wa walimu, wanafunzi na jamii au wanavijiji anasema Mwalimu Mkuu Ridhiwani Mfinanga.

Anaeleza kuwa tangu ahamie katika shule hiyo mwaka 2023 amefanya juhudi nyingi kutengeneza kumaliza utoro uliokuwepo na kuinua ufaulu wa shule hiyo, ambayo sasa inaanza kung'ara.

Anafafanua:"Niliwafuatilia wanafunzi vinara wa utoro na kuzungumza nao kuelezana sababu ili niweze kutafuta ufumbuzi kwa kutumia vyanzo halisi."

Anasema amewarejesha wanafunzi 10 wa darasa la saba shuleni ambao hata hivyo katika mtihani wa taifa hawakufanya vizuri japo wamepata vyeti vya kuhitimu mwaka 2023.

Mwalimu huyo anasema mwaka 2023 waliohitimu elimu ya msingi Bokotimiza walikuwa 79 kati yao 69 walifaulu, mwaka 2024 wanafunzi 94 walihitimu 86 walifaulu na ni kipindi ambacho shule hiyo iliondoka kwenye kundi la kuwa wa mwisho ngazi ya halmashauri na sasa ni miongoni mwa vinara ikielekea kufika 10 bora.

"Tulianza kuondoka kwenye nafasi ya mwisho pamoja na kuendelea kuwa na ufaulu wa wastani wa daraja C ukilinganisha na ilivyokuwa awali."

Anasema ufaulu huo ni matokeo ya juhudi za kudhibiti utoro na pia kuongeza ushirikiano baina yao na wazazi,walezi na jamii.

"Awali wazazi na walezi wakiitwa hapa shuleni walikuja kwa shari kama vile walimu ni adui zao hali hii tumeibadilisha na sasa wananchi, wazazi wa wanafunzi na walimu tumeimarisha ushirikiano kila jambo tunajadili kwa pamoja na kulitafutia utatuzi," anasema Mfinanga.

Mbali na hayo anaeleza kwamba kushuka kwa ufaulu kulichangiwa na njaa na hivyo wameanzisha utaratibu wa chakula ambacho wanafunzi wanachangia Sh. 500 kila siku ili wapate chakula jambo ambalo wameafikiana na wazazi na linaendelea kutekelezeka.

> Katika shule hiyo matokeo mabaya yanaelezwa kwamba yalipatikana mwaka 2019, 2020 na mingine ya nyuma lakini kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2022 hali imeanza kubadilika kwa kuondoka kwenye matokeo ya shule 10 duni za halimashauri hiyo.

"Njaa ilikuwa inashusha ufaulu kwakuwa wanafunzi wanaingia asubuhi hadi mchana hawajala chochote. Ukifundisha wakiwa na njaa hawakuelewi. Tumeanzisha utaratibu wa chakula na sasa tunashuhudia mabadiliko. Shule nyingine naomba ziige tunachofanya," anasema Mfinanga.

Sambamba na yaliyofanyika katika kuinua ufaulu na kudhibiti utoro, Mfinanga anaishukuru serikali kwa kutoa fedha za ukarabati wa vyumba vya madarasa vilivyokuwa vimechakaa.

Shule hiyo ina wanafunzi 735 tayari 698 wameripoti tofauti na miaka mingine ambapo kipindi kama hicho asilimia kubwa walikuwa bado nyumbani.

Shule hiyo pia ina uhitaji wa madawati 56 kati ya 266 yanayohitajika, nyumba sita za walimu zilizopo ni nne, vyumba vya madarasa ni saba kati ya 11 vinavyohitajika pamoja na matundu ya vyoo 18 ukilinganisha na yaliyopo sita kati ya 24 yanayohitajika.

Mmoja wa walimu wa shule hiyo Felista Msemwa, anasema awali wazazi walikuwa hawana mwamko wa kuwahamasisha wanafunzi kwenda shule zinapofunguliwa tofauti na sasa.

Anasema utoro wa mwaka 2023 na miaka mingine ya nyuma ulikuwa mkubwa tofauti na sasa na pia wanafunzi waliokuwa wanaripoti kwa wakati wakiwa na vifaa vyote vinavyotakiwa yakiwamo madaftari.

"Wazazi na walezi wengi walikuwa hawawahishi wala kuhimiza watoto wao umuhimu wa shule. Walijenga dhana kwamba siku za mwanzo ni za kufanya usafi na hakuna ratiba za masomo, inaweza ikatokea mfano kati ya wanafunzi 700 siku ya kwanza wanaweza wakaripoti100 pekee tofauti na mwaka huu ambapo siku ya kwanza walifika 600 kati ya 735," anaeleza Felista.

Aidha, anasema mbali ya mwamko huo wa wanafunzi kuripoti shule kwa wakati pia wanafika wakiwa na vifaa vyote vinavyotakiwa ikiwemo daftari na kalamu jambo ambalo ni mabadiliko makubwa yaliyofanyika kutokana na kuimarisha ushirikiano.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule Ramadhani Mkweche, anaeleza kwamba kamati yao katika kuboresha miundombinu imeanza na kukarabati miundombinu ya maji shuleni na kuunganisha umeme.

Mkweche anasema wamekubaliana na wazazi kuendelea kushirikiana kwa michango mbalimbali kujenga maboma ya vyumba vya madarasa ili serikali iweze kuyamalizia na kupunguza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa."anasema.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo Najma Bakari pamoja na Dickson Christopher, wanasoma darasa la saba wanashukuru serikali kwa kuboresha miundombinu ya madarasa pamoja na madawati.

Ajuaye Mohamed mmoja wa wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo anaeleza kwamba mabadiliko yaliyofanyika yataongeza ufaulu kwa wanafunzi shuleni.

Ajuaye anasema awali wanafunzi ikifika saa nne asubuhi walionekana mitaani wakizurura bila sababu na wengine hawakwenda shule jambo lililochangia kupata matokeo mabovu.

Kwa upande wake Omari Mpoto, ambaye pia ni mkazi wa Bokotimiza anasema ufaulu umeongezeka ukilinganisha na miaka ya nyuma hali hiyo imechangiwa na ushirikiano wa karibu kati ya wazazi, walezi na walimu.

Pia anasema uelewa wa umuhimu wa elimu kwa watoto umekua na kuongezeka hivyo wazazi wengi sasa wanawafuatilia na kutafuta mafanikio na maendeleo ya watoto wao.

Katika shule hiyo matokeo mabaya yanaelezwa kwamba yalipatikana mwaka 2019, 2020 na mingine ya nyuma lakini kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2022 hali imeanza kubadilika kwa kuondoka kwenye matokeo ya shule 10 duni za halimashauri hiyo.

Pamoja na kuanza kwa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa wananchi wanaomba kuungwa mkono na wadau wa ndani na nje ya kata hiyo kuyakamilisha na kuondoa msongamano wa watoto darasani.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

UKIWA HAPA UTAPOFUKA

# Stendi, gereji, foleni barabarani, ndani ya lori

WAKAZI mijini karibu na barabara zenye foleni, wanaokaa vituo vya mabasi kupiga debe na wanaofanyakazi kwenye gereji jueni kuwa yajayo yatawasikitisha.

Ni kwa sababu moshi wa dizeli unaotoka kwenye injini unasababisha upofu na huenda ukikaa kwa muda mrefu utakuwa kipofu kutokana na wingi wa moshi huo, unaoathiri hata madereva pia.

Utafiti na ripoti kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), unasema kuwa moshi wa injini za magari unahusishwa na hatari kubwa ya kuongeza upofu.

Hali ya kupoteza kwa kiasi kikubwa uwezo wa jicho wa kuona, unatokana na vichafuzi vya hewa kama vile chembe chembe na gesi ya 'naitrojen dayoksaidi' inayopatikana katika moshi huo wa injini.

Kwa hiyo kwa wakazi wa miji na majiji mengi ya Tanzania ambako foleni ni jambo la kawaida, au kufanya kazi katika maeneo yaliyo na moshi mwingi wa magari kama vituo vya mabasi au barabara zenye msongamano kuna hatari maradufu ya kuwa kipofu uzeeni au baada ya miaka 50.

Pamoja na hayo, kufanyabiashara kwenye vituo vya mabasi na watoto mgongoni au kuwatandikia chini wacheze au kulala hakuwaachi salama.

Ni jambo la kuepuka kwa sababu ya kumharakishia mtoto upofu.

WHO inasema ni kwa sababu moshi wa magari huharibu retina na mishipa ya kuona ambayo ni sehemu ya jicho inayowezesha binadamu kuona.

Retina na 'optic nerve' ndizo zinazoathirika moja kwa moja kutokana na moshi wa dizeli, utafiti huo ukieleza kuwa hata kuwa au kufanyakazi kando ya barabara si salama.

Baadhi ya barabara zenye foleni kama za Mandela, Morogoro, kituo cha mabasi cha Magufuli na vituo vingine kama Mbezi, Mbagala, Makumbusho vyote vya Dar es Salaam, si sehemu salama kuna hatari ya upofu.

Tatizo la macho linaanza kuwanyemelea kuanzia miaka 45 na kuendelea.

Kwa upande wa Iringa kipande cha kutoka Mahenga hadi Ilula nacho kuna foleni inayosababishwa na Mlima Kitonga, wasafiri na wasafirishaji wakielezwa kuwa wanakaa kwenye foleni hata zaidi ya saa tatu.



Kufanya shughuli pembeni ya barabara zenye foleni ni chanzo cha upofu. **PICHA: MTANDAO**

Moshi wa magari huchangia kwa kiwango kikubwa kwa ugonjwa unaofahamika kama Age-Related Macular Degeneration (AMD) ambao husababisha watu wa kuanzia miaka 45 kupoteza uwezo wa kuona, inasema WHO.

Wakazi wa mijini wanaofanya mazoezi pembeni ya barabara hawako salama wanaambiwa kuwa wanajiletea shida ya macho kiasi miaka inavyokwenda.

Ugonjwa wa upofu uzeeni awali ulihusishwa na kuvuta sigara lakini pia unaweza kuwa sawa na moshi wa magari ambao una madhara sawa na sigara kwenye kudhuru macho.

Moshi unaotolewa na magari umejaa 'kaboni monooksaidi, naitrojeni oksaidi' na kemikali nyinginezo zilizoko kwenye dizeli na petroli ambazo zinahusishwa na kusababisha maradhi mbalimbali pamoja na saratani.

WHO inakadiria kuwa moshi wa magari huchangia zaidi ya asilimia 25 ya saratani ya mapafu na magonjwa mengine ikiwamo pumu au asthma.

Kwa mujibu wa mtandao wa 'American Cancer Society,' katika tafiti za seli zinazofanyika maabara, moshi wa dizeli , pamoja na masizi na kemikali nyingine unasababisha mabadiliko katika nasaba za viumbe hai (DNA) za seli.

> Kwa hiyo kwa wakazi wa miji na majiji mengi ya Tanzania ambako foleni ni jambo la kawaida, au kufanya kazi katika maeneo yaliyo na moshi mwingi wa magari kama vituo vya mabasi au barabara zenye msongamano kuna hatari maradufu ya kuwa kipofu uzeeni au baada ya miaka 50.

Kubadilisha utaratibu wa chembe hai na kuanzisha saratani mwilini kwani udhaifu wa seli au DNA huchochea mwili kuwa kinyume na utaratibu wake asilia.

DNA inapovurugwa husababisha chembe zenye saratani kukua, ingawa sio vitu vyote vinavyosababisha mabadiliko ya DNA pia husababisha saratani.

Tafiti kadhaa zinagundua kuwa kuvuta kwa muda mrefu moshi mzito wa dizeli kunaweza kusababisha saratani ya mapafu kwa wanyama wa maabara kama panya, hivyo hali hiyo hutokea kwa binadamu.

Aidha, tafiti kadhaa zimegundua kuwa kuna uhusiano kati ya moshi wa dizeli na saratani nyingine, ikiwa ni pamoja na kansa ya kibofu cha mkojo.

Nyingine ni ya 'larynx' au sanduku la sauti koromeo, tumbo na kongosho. Uchunguzi pia umehusisha saratani ya mfumo wa damu kama vile 'lymphomas na lukemia' pamoja na lukemia kwa watoto kuwa chanzo ni moshi wa dizeli.

Kwa mtaji huo sekta ya usafiri huchangia asilimia kubwa ya vifo vyote vinavyotokana na hewa chafu ya dizeli.

Pamoja na changamoto hiyo Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), linaeleza kuwa, kuvuta mara kwa mara hewa chafu au moshi wa injini za magari zinazotumia dizeli kuna uwezekano wa kuugua maradhi ya kusahau au 'dimensia'.

Ni wazi kuwa kama juhudi hazitafanyika na kubadilisha injini ili zitumie nishati safi kuna uwezekano madhara yanayosababishwa na moshi wa magari kuongezeka maradufu kwa muda mfupi.

UNEP inasema ni kwa sababu ununuzi wa magari ni mkubwa na hata yale yaliyotumiwa kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Mataifa yanayoendelea ya Afrika usajili wa magari ni mkubwa kwa sababu watu hununua magari kila uchao.

Lakini magari yanayonunuliwa kila siku na uchache au uhaba wa miundombinu umesababisha foleni barabarani na kuathiri afya za watu na hali ya hewa angani kwa sababu inaongeza joto zaidi.

Wakati umefika wa sheria kuelekeza polisi kuondoa magari ya usafiri wa umma, malori ya shehena na hata ya watu binafsi yanayotoka moshi ili kuwanusu watu na janga la moshi wa dizeli.



## Wafanyabiashara walilia pensheni

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAFANYABIASHARA mkoani hapa wameitaka serikali kuweka utaratibu wa kuwalipa pensheni kwa kulipa kodi kwa uaminifu baada ya kuzeeka.

Wafanyabiashara hao walitoa rai hiyo juzi wakati wa kikao cha Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi cha kupokea malalamiko, changamoto na mapendekezo wanazokumbana nazo.

Philemon, alisema iwapo serikali itaweka utaratibu huo itatoa hamasa na ari kwa wafanyabiashara kulipa kodi kwa moyo kwa kuwa wanafahamu uzeeni watanufaika na pensheni kama kwa watumishi.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Wilaya ya Ikungi, Kulwa Kasule, alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wanasiasa wanapoona wafanyabiashara wanagombea ubunge kuwachongea Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili wakadiriwe na kutozwa kodi kubwa kama njia ya kuwakomoa.

Wafanyabiashara hao, walisema utitiri wa kodi kwa wafanyabiashara ni moja ya changamoto inayosababisha kukwepa ulipaji kodi stahiki.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue, alisema lengo la kuchukua maoni na mapendekezo ya wafanyabiashara hayo ni kuwasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili kupatiwa ufumbuzi.

Katibu Tawala Mkoa wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, aliwataka wafanyabiashara wa mkoa huo kuendelea kutoa maoni na mapendekezo ya maboresho ya kodi kupitia kwenye tovuti.

## Halmashauri zakumbushwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) imezitaka halmashauri nchini kutekeleza agizo la serikali la kutafuta vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Murshid Ngeze, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mkutano mkuu wa jumuiya hiyo unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao jijini Mwanza.

Ngeze, alisema agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Omary Mchengerwa, kwenye Mkutano Mkuu wa ALAT, uliofanyika mwaka jana visiwani Zanzibar.

"Katika mkutano ule waziri aliagiza kuwa halmashauri zote nchini kuhakikisha zinabuni vyanzo vipya viwili ili kuongeza ukusanyaji mapato ambayo yataongeza wigo wa utelezaji wa miradi ya maendeleo.

Akizungumzia kuhusu mkutano mkuu wa ALAT, alisema umepangwa kufanyika kuanzia Februari 17 hadi 21 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi.

# Aliyekuwa dereva wa Mbowe amwangukia Tundu Lissu

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Jimbo la Singida Mjini, Shwahib Mohamed, amemwomba Mwenyekiti mpya wa Taifa wa chama hicho, Tundu Lissu kuvunja makundi yote yaliyojitokeza wakati wa mkutano mkuu wa chama.

Mohamed ambaye alikuwa mlinzi wa Mwenyekiti mstaafu wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema jana mjini hapa kuwa baada ya uchaguzi, makundi yote yaliyokuwapo yanapaswa kuvunjwa ili kujenga chama kiwe imara kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu

"Japokuwa mimi nilikuwa upande wa kundi lililokuwa linamuunga mkono Mbowe, ninampongeza Lissu na Makamu Mwenyekiti, John Heche kwa ushindi waliopata katika uchaguzi ambao ulikuwa huru na haki. Tunachoomba hawa wawe mstari wa mbele sasa makundi yasiwamo ndani ya chama," alishauri.

Alisema wanachama wana matarajio makubwa sana na uongozi wa Lissu kuleta mabadiliko chanya yatakayoleta upinzani wa dhati na kujihakikishia kushika dola katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

"Mwaka huu ni wa uchaguzi. Mshikamano mkubwa unahitajika kwa viongozi na wanachama wote na hiyo ndiyo itakuwa silaha kubwa ya kupata ushindi," alisema.

Januari 9 mwaka huu, Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Omari Toto, aliitisha kikao cha viongozi na kutoa tamko kuwa mkoa utamuunga mkono Lissu katika uchaguzi wa viongozi wakuu wa chama uliofanyika Januari 21 mwaka huu.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Singida Mjini, Mohamed, aliibuka na kupinga hatua hiyo, akidai kuwa si kweli kwamba wajumbe wote wa Mkutano Mkuu kutoka Singida walikuwa wanamuunga mkono Lissu.

"Mkutano tulioitiwa na Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa tuliambiwa ni wa mashauriano lakini kwa sababu akidi ya wajumbe haijatimia, tumeshangaa mwenyekiti anaita waandishi wa habari na kutoa tamko kwamba CHADEMA Mkoa wa Singida wanamuunga mkono mgombea uenyekiti Tundu Lissu," alisema.

Kwa mujibu wa Mohamed, kati ya wajumbe wa Mkutano Mkuu 29 wanaotoka mkoani Singida, 20 walikuwa wanamuunga mkono Mbowe katika uchaguzi huo.

Lissu alitangazwa mshindi wa kinyang'anyiro hicho akipata kura 513 dhidi ya 482 za Mbowe na moja ya Odero Charles.




Rais mstaafu, Dk Jakaya Kikwete akiangalia mtambo katika maabara maalumu ya moyo (Cathlab), alipotembelea Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Prof. Abel Makubi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jakaya Kikwete ajivunia maono BMH

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete amesema anajivunia ndoto yake kuendelea kutimia katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) ya kuifanya kuwa kituo cha umahiri cha matibabu ya figo na huduma nyingine za kibingwa nchini.

Kikwete aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kutembelea hospitali hiyo iliyopo jijini Dodoma.

Alisema miaka ya nyuma wananchi walikuwa wanapata shida ya kupata huduma za matibabu ya figo, uchujaji wa damu na baadhi kulazimika kwenda katika Jiji la Nairobi nchini Kenya ili kunusuru maisha yao.

"Maono yangu wakati tunaanzisha BMH ilikuwa kuanzisha hospitali ambayo itakuwa kituo cha umahiri nchini katika matibabu ya figo na huduma zingine za ubingwa wa juu, nimefurahi kuona hayo yanafanyika, " alisema Kikwete.

Alifafanua kuwa amefurahishwa kuona ndoto yake inatimia kwa sababu kwa sasa BMH inatoa huduma za kibingwa za matibabu ya figo, uchujaji wa damu na upandikizaji figo nchini.

"Pamoja na hatua hiyo kubwa ambayo imefikiwa, haizuii BMH kuwekeza katika utoaji huduma za matibabu ya magonjwa mengine," alisema na kuongeza kuwa:

"Hii ni hospitali ya nyota tano tulipanga iwe kituo cha umahiri kwenye matibabu ya kibingwa kama figo, lakini tulitaka itoe matibabu mengine ya ubingwa wa juu na imesadifu hayo maono."

Alisema amefarijika pia kushuhudia huduma za hali juu katika uchunguzi na tiba ya moyo na upandikizaji uloto zinazoendelea kutolewa hospitalini hapo.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Profesa Abel Makubi, alisema hadi sasa wagonjwa 50 wamepandikizwa figo tangu huduma hiyo ilipoanzishwa hospitalini hapo.

Prof. Makubi, alisema tangu kuanza kutoa huduma hiyo nchini, wameokoa kiasi cha Sh.bilioni 1.6 ambazo zingetumika kuwapa rufaa wagonjwa kwenda nje ya nchi kwa upandikizaji wa figo.





# DC awapa mbinu wafanyabiashara kuinua vipato vyao

**Na Mwandishi Wetu,** CHUNYA

WAFANYABISHARA wadogo wilayani Chunya mkoani Mbeya, wametakiwa kutumia vema fursa zinazopatikana kupitia mfumo mpya wa vitambulisho vya kidijitali vinavyotolewa kwa wajasiriamali ili waweze kuinua kipato chao.

Mkuu wa wilaya ya Chunya, Mbarak Batenga alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akitoa elimu kuhusu faida mbalimbali watakazozipata wafanyabiashara hao baada ya kujisajili kwenye mfumo mpya wa kupata vitambulisho hivyo.

Alisema vitambulisho hivyo vitawezesha wajasiriamali kutambulika rasmi na kupata fursa za kibiashara zilizopo ikiwemo mikopo kutoka serikalini pamoja na taasisi mbalimbali za kifedha.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameandaa programu maalumu ya kuwakopesha wajasiriamali watakaokuwa wamesajiliwa na kupata vitambulisho hivi na ukomo wa mkopo unakwenda mpaka shilingi milioni nne sasa ni juu yenu utakopa shilingi ngapi kulingana na mahitaji yako," alisema Batenga.

Alisema awali vitambulisho vya wajasiriamali vilisimama kwa muda kabla ya kurejeshwa tena na kwamba kwa sasa vimerejeshwa kwa mfumo ulioboreshwa zaidi ikiwa ni pamoja na kuunganishwa na mfumo wa kibenki kwa lengo la kuwawezesha wajasiriamali kukopesheka na taasisi hizo.

Alisema pia vitambulisho hivyo vimeunganishwa na kitambulisho cha NIDA kwa lengo la kupata taarifa za mjasiriamali zitakazomtambulisha rasmi ili aweze kunufaika na fursa zinazotolewa na serikali kupitia taasisi za kifedha kama vile mikopo yenye riba nafuu.

Alisema lengo la serikali kuwezesha wajasiriamali hao ni kuwatoa kwenye mikopo umiza na kwamba wilaya hiyo inatamani kuona watakaopata mikopo hiyo wakifanikiwa kutoka kuwa wafanyabishara wadogo na kuwa wafanyabiashara wakubwa watakaoinua na wengine.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Chunya, Elizabeth Lusale alisema Rais Samia aliamua wafanyabiashara wadogo kuwa kundi maalumu chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, hivyo watahakikisha wanatimiza adhima hiyo ya kuwawezesha kiuchumi.

## Wakazi Njombe watakiwa kushiriki hafla za kisheria

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI mkoani Njombe wameshauriwa kuona umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika masuala ya kisheria ili kufahamu haki na wajibu wao.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari wakati wa uzinduzi wa wiki ya sheria iliyofanyika katika viwanja vya stendi ya zamani mjini Njombe.

Uzinduzi huo uliambatana na matembezi ya hiyari yaliyowashirikisha wananchi, wadau wa sheria, wanafunzi, pamoja na viongozi wa serikali kutoka ngazi mbalimbali.

Judica alisema wiki ya sheria ni fursa muhimu kwa wananchi kupata elimu ya kisheria, kujua haki zao na namna ya kuzitetea.

Judica alisema katika wiki hiyo, wananchi watapata nafasi ya kupata msaada wa kisheria kutoka kwa wanasheria na mawakili, huku wataalamu wa sheria wakitoa elimu kuhusu umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya sheria na matumizi ya mabaraza ya usuluhishi.

Mratibu Msaidizi Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) Mkoa wa Njombe, Innocent Kibadu alisema katika wiki hiyo pamoja na mambo mengne pia watatoa elimu kwa wananchi juu ya kujua taratibu za mirathi kwa sababu ni moja yya tatizo hivi sasa.

Mmoja wa wananchi mjini Njombe Sara Sanga alisema bado wananchi hawana uelewa wa kutosha kuhusu sheria, hivyo bado elimu inahitajika ili waweze kuwa na uelewa utakaowasaidia katika uamuzi.

Wiki ya sheria ni maadhimisho ya kila mwaka yanayoandaliwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya sheria, ikiwa na lengo la kuelimisha wananchi kuhusu haki zao na kuwahamasisha kushiriki katika mifumo ya utoaji wa haki.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA

(AT ARUSHA)

CRIMINAL CASE NO. 25584 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

YUSUF MOHAMED KONDO..........................ACCUSED PERSON

To:
Yusuph Mohamed Kondo
Plot No. 92, Block X, Area F
Arusha City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 31st day of January 2025 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 6TH day of JANUARY, 2025

..........................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name..........................
Signature..........................
Qualification/Relationship
Date..........................

183427

CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MOROGORO

(AT MOROGORO)

CRIMINAL CASE NO. 31063 OF 2024.

THE REPUBLIC

VERSUS

FAIZA MUSSA MUSTAFA .......................... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)

To: Faiza Mussa Mustafa of Plot No. 1033, Block L, Kingolwira Area, Morogoro Municipality

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person (or by Advocate, as the case may be) before this Court on the 25 day of JANUARY 2025

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 20TH day of DECEMBER 2024

..........................
Resident Magistrate
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO

183427



# Naibu Spika ahimiza utoaji elimu yenye viwango

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Bazara la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma amesema wadau sekta ya elimu wanawajibu wa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa Zanzibar inakuwa na ubora na inakidhi mahitaji ya vijana.

Alisema hayo juzi katika mahafali ya sita ya Chuo cha Microtech Institute of Business and Technology.

Alisema kuwa kuna haja sekta binafsi kushirikiana na serikali kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za jamii hasa katika elimu na kubuni masomo au kozi ambazo zitaongeza thamani katika ujenzi wa taifa.

Alisema kuwa katika kufikia malengo ya kuanzishwa kwa vituo hivyo vya chuo vinavyotoa elimu ni lazima walimu kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha suala la ubunifu linapewa nafasi katika chuo hicho ili kuwa chachu ya maendeleo kwa wanafunzi wa chuo hicho.

Alisema kuwa walimu wa vyuo wanawajibu wa kuwafundisha vijana masomo ya kujiajiri baada ya kumaliza masomo yao na siyo kusubiria ajira kutoka serikalini.

"Utamaduni wa ujasiriamali lazima upewe nafasi katika mchakato mzima wa elimu ili kuwawezesha wanafunzi wanapomaliza masomo wawe na uwezo wa kujiajiri" alisema Naibu Spika.

Kadhalika, alisema kuwa baadhi ya wanafunzi katika chuo hicho wameanza kusajili kampuni zao kwa mwongozo wa walimu wenye uzoefu hatua ambayo ni ya kusifiwa na kupigiwa mfano kwa wanafunzi hao.

Alisema kuwa maendeleo ya Zanzibar yatapatikana ikiwa kutakuwa na nguvu kazi yenye ujuzi na uzoefu katika masula mbalimbali hasa ya elimu yenye manufaa kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa sekta zote za kiuchumu na kijamii zinahitajika watendaji wenye taaluma ya hali ya juu ili kukuza fani na tija ya uzalishaji mali na utoaji wa huduma.

Alisema kuwa licha ya wanafunzi hao wa shahada na stashahada kumaliza masomo yao lakini bado wana nafasi ya kuendelea kusoma ili kuendana na soko la ajira.

Mkuu wa chuo hicho, Farihiya Mohammed Ali, alisema kuwa wanafunzi 240 wamehitimu mafunzo katika kada mbalimbali ikiwemo ya upishi, ushonaji, ugavi na manunuzi, uwalimu pamoja na Tehama.

Alisema kuwa licha ya kuwepo kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika chuo hicho lakini kinakabiliwa na changamoto ya kutoshirikishwa katika mabadiliko ya sera kulingana na wakati uliopo kwa wahusika .

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Zulfa Mohamed Ali alisema chuo hicho ni kimbilio kubwa kwa vijana katika kujifunza masomo ya fani mbalimbali ili kuendana na wakati uliopo na ushindani wa soko la ajira.

Alisema kuwa chuo hicho bado kinakabiliwa na uhaba wa vitabu vya kujifunzia kwa wanafunzi pamoja na changamoto ya kupatiwa mikopo kutoka serikalini kama vyuo vingine vya elimu ya juu.



Baadhi ya wananchama wa Umoja wa Wanaume Katoliki (UWAKA) wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Petro. wakichangaia damu salama kwa ajili ya kusaidia wengine ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Siku ya UWAKA 2025, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mtaalam wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Rajabu Kwese. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wampa kongole mkurugenzi ukusanyaji mapato

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro limepitisha azimio la kumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Khamis Katimba kwa utendaji uliosababisha kuongeza mapato ya halmashauri.

Walitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki katika kikao cha baraza la madiwani baada ya Diwani wa Kata ya Usangule, Nassoro Ligugula kupeleka hoja hiyo.

Ligugula alieleza kwa kina mchango wa mkurugenzi huyo tangu alipohamishiwa kwenye halmashauri hiyo miezi saba iliyopita.

Ligugula alisema mkurugenzi huyo amefanikiwa kubadili mifumo ya ukusanyaji wa mapato jambo lililosaidia kupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa asilimia 87 kwa miezi sita pekee.

"Mpaka sasa kwenye kipindi cha miezi hii sita pekee, fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi zimeshapelekwa kwa asilimia 87, bado asilimia 13 tu na kuna miezi sita mbele, ndiyo maana hapa tunajivuna kwasababu zamani haikuwa hivi," alisema

Alisema alikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo kwa miaka mitano, awali madiwani walikuwa wakipanda hadi kwenye meza kwa ajili ya kuvutana kuhusu miradi.

Alisema tangu mkurugenzi mpya (Katimba) aanze kuiongoza halmashauri hiyo miradi na viporo vyote kwa asilimia 90 imesha na mingine inamaliziwa.

Kabla ya Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Pius Mwelase kuwauliza madiwani ridhaa ya kupitisha azimio hilo, Ligugula alisema, hakuna serikali inayoweza kujiendesha bila ukusanyaji mzuri wa mapato na kwamba katika suala la mapato kwa sasa Malinyi wamefanikiwa.

Baada ya hoja hiyo, Mwenyekiti Mwelase aliwauliza madiwani wa baraza hilo kama wanakubaliana na hoja hiyo.

## Viongozi CCM, wadau watakiwa kuunga mkono miradi ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla amewataka viongozi wa CCM na wadau kujitolea katika kuchangia na kuunga mkono ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na chama pamoja na serikali.

Alitoa wito huo juzi alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) kinachojengwa eneo la Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja na kuchangia vifaa mbalimbali ili kuendeleza ujenzi huo.

Hemed ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alikabidhi mifuko ya saruji mifuko 1,000, gari 10 za mchanga na Sh. milioni tano zitakazosaidia katika kuwapatia huduma vijana na wale wanaojitolea katika ujenzi wa chuo hicho.

Alisema CCM na serikali wanatambua kuwa nguvu na mchango wa vijana wa UVCCM katika kukijenga na kukiimarisha chama hasa katika kusimamia ujenzi wa chuo cha UVCCM kitakacho wafundisha vijana kuwa watiifu na wazalendo kwa taifa pamoja na kuwafundisha namna ya kujitegemea kiuchumi.

Hemed alisema kuwa changamoto zinazowakabili UVCCM hasa katika ujenzi wa chuo hicho serikali itazifanyia kazi ili kufanikisha malengo ya ujenzi huo kwa maslahi ya CCM.

Aidha, alisema kuwa amefarajika kuona kazi kubwa inayofanywa na vijana wa UVCCM ya kujitolea katika kukiendeleza na kukijenga chama.

Aliwataka vijana kuendelea kuitunza amani iliyopo nchini hasa katika kupindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na kuwaahidi kuwa watahakikisha chuo hicho kinamalizika katika viwango vyenye ubora na hadhi ya hali ya juu kwa maslahi mapana ya vijana wa CCM na Taifa.

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mohamed Ali Kawaida, alisema dhamira ya ujenzi wa chuo hicho ni kuendelea kutengeneza makada wa CCM na viongozi wenye uchungu na uzalendo wa nchi yao pamoja na kuwafunza namna bora ya kujiendeleza kiuchumia katika harakati zao za maisha.

Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Zanzibar, Abdi Mahmoud Abdi alisema kumalizika kwa ujenzi wa chuo hicho kutawanufaisha vijana ambao watapatiwa mafunzo mbalimbali yakiwemo ya uzalendo na stadi za maisha.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**DENNIS NEMES MALEKANI** anatangaza kupotelewa na vyeti. University Transcript na University Certificate in Doctor of Medicine vyenye Index namba **2015-04-08617** vilivyotolewa na Muhimbili University of Health mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/279665/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAIKO ELETELIUS MLELWA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 538 DLN - TOYOTA BREVIS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **NJR/TR/RB/16/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MASERO JAMES MAHENDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 425 BYU - MITSUBISH PAJERO** yenye Chassis namba **H57A0035002.** Engine namba **4A31629425.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MAR/TAR/447/2025.**

## KUPOTEA KWA NYARAKA ZA KIWANJA

**ELIAS SIMON NDAJI** anatangaza kupotea kwa nyaraka ya umiliki kiwanja the Registered Trustees Of Kanisa la Pentekoste namba **579 Kitalu"EE"** Ngokolo Shinyanga Manispaa. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/SHI/3599/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASIFIWE HASHIM MNDOLWA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Toyota Cami** yenye namba za usajili **T405deb,** Chassis namba **J102E008732,** Engine namba **K3EAA8732** yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ /DOD/DOD/2628/2025**

## KADI ZA PIKIPIKI ZIMEPOTEA

**JOHN SAMSONI JOHN** anatangaza kupotelewa kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 167 CKE, MC 996 CPV, MC 451 CQB na MC 943 DPM** zote aina ya **TVS.** Yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **PHQ/DAR/KIN/11679/2025.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:- 1.2025**

**MDAI:- RHOBYNER ENOS PIUS.**

**DHIDI YA**

**MDAIWA:- GODFREY JOSEPH MPONDA.**

**Kwa:- GODFREY JOSEPH MPONDA.**

**Ombi la mdai:-**
**Madai ya Talaka kwa ajili ya kusikiliza.**
**Madai ya :- Madai ya Talaka.**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 05 mwezi 02 mwaka 2025 Saa 2:30 Asubuhi.
Angalia kama *hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 27 mwezi 01.2025.

MOROGORO.
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1050 OF 2025**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PETER BUSORO MAUGGO**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY**

**JUDITH ALEXANDER RUSHOHORA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 19 day of 02...................... 2025
Dated at Dodoma this 27 day of January.............2025

........................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 371 of 2025**

**In the matter of the estate of the late ARNOLD ELIA LYIMO of MBWANGA within Dodoma City**

**And**

**In the matter of an application for letters of administration by FLORIDA HENDRY NJAU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 27 day of 2............................2025

Dated at Dodoma this 27 Day of 1................2025.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOYCE CHARLES ATHANAS,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Toyota IST** yenye namba za usajili **T 922 DGX, Toyota Vanguard** yenye namba za usajili T 613 EDV. Yeyote akaeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/2348/2025.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya Shinyanga**
**Kituo cha Mjini Mkoa wa Shinyanga**

**Shauri la Madai Na 06/2025**
**Jina la Mdai RAPHAEL GURTI**
**Jina la Mdaiwa MOSSI NURI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 kanuni za taratibu Madai katika Mahakama ya Mwanzo) kwa MOSSI NURI**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba unadaiwa kiasi cha Tshs 1,773,294/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 6 mwezi 2 mwaka 2025 saa 8:00 asubuhi,kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili, ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**Angalizo:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo
Hati hii imetolewa na Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17 mwezi 01 mwaka 2025

HAKIMU
SAHIHI YA MPOKEAJI.......................
SAHIHI YA MWASILISHAJI....................... TAREHE......

**HAKIMU**

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 126/2025**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MAUA DAUDI MHINA WA KISIWANI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HARUNA RAMADHANI AMRI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 mwezi 02 mwaka 2025 saa 2:00 asubuhi kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetokewa leo tarehe 22 mwezi 01 mwaka 2025.

HAKIMU

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1617 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PAULINA LAZARO NAMRIBA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ALBERT ZABRONI KUBWALAO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 day of February, 2025.
Dated at **KOROGWE** this 22 day of January, 2025.

RESIDENT MAGISTRATE

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Tibaijuka: Uamuzi wa Trump hatari Afrika, AU iketi haraka

**Na Maulid Mmbaga**

ALIYEKUWA Naibu Katibu Mkuu katika kitengo cha Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi (UN-HABITAT) Prof. Anna Tibaijuka ameishauri Wizara ya Afya kuchukua hatua zaidi ya maamuzi yaliyochukuliwa na Rais wa Marekani, Donald Trump wa kusitisha misaada kwa mashirika ya afya duniani.

Kiongozi huyo mpya wa Marekani baada ya kuingia madarakani amesaini nyaraka mbalimbali za maamuzi zikiwemo kuondoa taifa hilo katika uanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na kusitisha misaada kwa mashirika ya afya duniani hasa PEPFAR na Global Health Fund.

PEPFAR ni Mpango wa Dharura ulioundwa na Rais George Bush mwaka 2003 kukabiliana na UKIMWI na inatoa dawa za ugonjwa huo kwa zaidi ya watu milioni 20.6, kuwaweka wagonjwa hai na kuwazuia kusambaza virusi.

Kupitia andiko alilolichapisha jana kwenye ukurasa wake wa X, Prof. Tibaijuka aliandika kuwa endapo uamuzi huo wa Rais Trump utatekelezwa itakuwa ni kiama kwa Watanzania na Afrika kwa ujumla, akihadharisha kuwa upatikanaji wa dawa ya kuongeza kinga za mwili (ARVs) utaathirika.

"Ninashauri Wizara ya Afya kuufahamisha umma wa Watanzania je ni hatua gani za haraka zinachukuliwa kutathmini jambo hili na kuchukua hatua stahiki?," aliandika Prof. Tibaijuka.

Prof. Tibaijuka ambaye pia aliwahi kuhudumu katika ofisi kuu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) mjini Geneva, alishauri Umoja wa Afrika (AU) kuitisha kikao maalum kuangalia swala hilo na kuweka mkakati wa pamoja.

Alisema waathirika wa ugonjwa huo wa Kukosa Kinga Mwilini (UKIMWI) ni Waafrika licha ya kwamba haujulikani ulikotoka, huku akisisitiza kuwa ni muhimu kujitetea.



Aidha, alisisitiza kuwa juhudi za kudhibiti maambukizi ya Virus vya Ukimwi (VVU) ziwekewe nguvu mpya, kwakuwa upatikanaji wa ARVs utakuwa mgumu. Na kwamba kununu dawa hizo kibiashara ni jambo litakalohitaji bajeti kubwa na licha ya uwezo wa taifa kuwa mdogo.

"Jambo hili limekuwa la ghafla, waathirika wengi hawana uwezo kununua madawa hayo wenyewe maisha yao yote, afya zao zikidhoofika itatumika gharama kubwa kuwauguza hivo kusababisha umaskini na vifo. Pia bila ARVs maambukizi yatashika kasi mpya. Tuwe macho," alishauri Prof. Tibaijuka.



Wakazi wa Mji wa Goma mashariki mwa DRC wakikimbia makazi yao kutokana na machafuko yanayoendelea baada ya mji huo kutekwa na Waasi wa M23, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Hali yazidi kuwa tete DRC

## • Ruto aingilia kati

**Na Maulid Mmbaga**

WAASI wa M23 wamedai kuwa wameukamata mji mkubwa wa kibiashara wa Goma nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na kuwahimiza wakazi wa kuwa watulivu huku wakiwataka wanajeshi wa Congo kujisalimisha.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya M23 iliyotoka jana, ikiwa ni dakika chache kabla ya kumalizika muda wa saa 48 uliowekwa na waasi hao kwa Jeshi la Congo kusalimisha silaha zao.

Licha ya waasi hao kuwahimiza wananchi wa Goma kuwa watulivu, wamewataka wanajeshi wa Congo kukusanyika katika uwanja mkuu wa michezo, huku Shirika la Human Rights Watch likisema mzozo wa mashariki ya DRC unaweza kuwa janga la kibinadamu.

Msemaji wa serikali ya Congo, Patrick Muyaya anatoa wito wa ulinzi wa raia akisema nchi iko katika hali ya vita ambako habari zinabadilika kila wakati, huku ikielezwa kuwa walinda amani wa Umoja wa Mataifa (UN) walianza kuwasajili askari waliojisalimisha kwenye viunga vya mji huo.

Inadaiwa kuwa wakati wakisaidiwa na maelfu kadhaa ya askari wa Rwanda, waasi wa M23 katika siku za karibuni wamesonga mbele kwa kasi wakikabiliana na wanajeshi wa Congo wanaoulinda mji wa Goma.

Pia inaelezwa kuwa wanajeshi kadhaa wa kigeni wa kulinda amani wameuawa katika makabiliano hayo, na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres ameitaka Kigali kuwaondoa wanajeshi wake nchini humo, wito unaodaiwa kupuuzwa.

**INACHOSEMA RWANDA**

Katika taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Rwanda inasema inalazimika kuchukua hatua ya kuendelea kujihami na kujilinda kwa sababu ya mapigano yanayoendelea karibu na mpaka wake na DRC.



Kwenye kikao cha dharura cha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Waziri wa Mambo ya Nje wa Congo, Therese Kayikwamba Wagner anasema Rwanda inafanya uchokozi wa wazi, na kwamba ni tangazo la vita ambalo halijifichi tena nyuma ya ujanja wa kidiplomasia.

Vyanzo vya Umoja wa Mataifa vinaiambia AFP kwamba kati ya askari 500 na 1,000 wa Rwanda waliwasili Jumapili kujiunga na M23 karibu na Goma, huku Kayikwamba Wagner akitoa wito kwa baraza la usalama kuwawekea maofisa wa Rwanda vikwazo.

Inaelezwa kuwa Balozi wa Rwanda katika Umoja wa Mataifa Ernest Rwamucyo, hakuthibitisha au kukanusha madai hayo, licha ya kuilaumu serikali ya Congo, akisema mzozo huo ungeweza kuepukika kama ingeonesha dhamira ya kweli ya amani.

**BARABARA ZAFUNGWA**

Mwakilishi maalum wa Umoja wa Mataifa nchini Congo, Bintou Keita ameuambia mkutano wa dharura wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwamba wamewekwa kizuizini kutokana na uwanja wa ndege kufungwa na barabara kufungwa katika kitovu hicho kikubwa cha misaada ya kibinadamu na usalama katika eneo hilo.

Keita, anasema licha ya msaada wa askari wa kulinda amani kwa Jeshi la Congo, waasi wa M23 na askari wa Rwanda waliingia kitongoji cha Munigi, viungani mwa Goma, na kusababisha hofu kubwa.

Anasema wapiganaji wa M23 walikuwa wakisonga mbele kwa kuwatumia wakazi kama ngao ya binadamu, huku wengine wakikimbilia wakihofia juu ya usalama wao.

Hata hivyo, Baraza la Usalama linalaani kupuuzwa wazi wazi kwa uhuru na uadilifu wa mipaka ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Huku likiwataka wanajeshi wa nje waondoke, bila kuwataja moja kwa moja.

**WAFUNGWA WATOROKA**

Wakati huo huo, Shirika la habari la AFP linaeleza kuwa mamia ya wafungwa wametoroka katika jela moja iliyoko Goma, saa chache baada ya kuripotiwa kuwa waasi wa M23 na wanajeshi wa Rwanda, wameingia kwenye baadhi ya maeneo ya mji huo.

Vyanzo vya usalama vilivyonukuliwa na shirika hilo, vinadai kuwa gereza hilo lilikuwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa 3,000, na kwamba miundombinu yake ilichomwa moto, bila kueleza kwa kina kilichojiri.

Hayo yanaelezwa wakati serikali ya Rwanda ikisema imetuma mabasi kwenye mpaka wa nchi hiyo na DRC kwa ajili ya kuwaondoa wafanyakazi wa umoja wa Mataifa.

Hadi jana hakukuwa na taarifa rasmi kutoka kwa serikali ya Congo kuhusu kinachoendelea kwenye mji huo, huku Ufaransa ikitaka mashambulio ya M23 katika Mji wa Goma kukomeshwa.

Katika hatua nyingine, Rais wa Kenya William Ruto ametangaza mkutano wa kilele wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na viongozi wa Rwanda na DRC kuujadili mzozo huo. Akisema Rais wa Congo, Felix Tshisekedi na Paul Kagame wa Rwanda wamekubali kuhudhuria mkutano huo wa kilele utakaofanyika hivi karibuni.

**CHANZO: MTANDAO**

# TIMU 32 ZILIZOFUZU RAUNDI YA 4 KOMBE LA FA HIZI HAPA

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu nchini (TFF), limezitaja jumla ya timu 32 zilizotinga raundi ya nne ya michuano hiyo ambayo lengo lake ni kumsaka bingwa wa kuiwakilisha nchi kwenye kinyang'anyiro cha Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Taarifa iliyotolewa jana na TFF inaeleza kuwa timu hizo zitacheza raundi ya nne baada ya kuchezeshwa droo hivi karibuni, ambapo washindi watatinga hatua ya 16-bora.

TFF imetoa idadi hiyo ya timu baada ya kukamilika kwa mechi za raundi ya tatu, ambapo Simba na Yanga zilikamilisha raundi hiyo kwenye michezo yao ya viporo mwishoni mwa juma.

Awali, mechi hizo zilitakiwa kuchezwa Novemba, mwaka jana, lakini timu hizo zilikuwa kwenye harakati za michuano ya kimataifa, Yanga ikicheza Ligi ya Mabingwa Afrika na sasa imetolewa, Simba ikishiriki Kombe la Shirikisho na imefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali.

TFF imefanya hivyo siku moja tu baada ya Simba kuichapa Kilimanjaro Wonders mabao 6-0, mechi ikichezwa, Uwanja wa KMC Complex, siku mbili baada ya Yanga nayo kuichakaza Copco FC, mabao 5-0, mechi ikichezwa uwanja huo huo, uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Mbali na Simba na Yanga ambazo zilikamilisha raundi ya nne juzi, timu zingine zilizotiinga raundi hiyo kwa kushinda mechi zao za raundi ya tatu zilizochezwa mwishoni mwa mwaka jana ni, Green Warriors, TMA Stars, Mbeya City, Cosmopolitan, Polisi Tanzania, Stand United, Towns Stars, JKT Tanzania, Namungo FC, Mbambali Ushirikiano, Pamba Jiji, Transit Camp, Biashara United, KMC, Singida Black Stars, Mashujaa FC, na Coastal Union.

Zingine ni Leo Tena, Songea United, Mtibwa Sugar, Fountain Gate, Azam FC, Bigman FC, Kiluvya FC, Girrafe Academy, Geita Gold, Prisons, Kagera Sugar, Mbeya Kwanza, na Tabora United.

## NGOMA...



Kikundi cha ngoma za asili cha Nyati, kikipiga ngoma yao ya zeze na marimba, wakati kikitumbuiza katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ikungi kuboresha miundombinu ya michezo shuleni

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

SERIKALI kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, inatarajia kutoa jumla ya Sh. milioni 280, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya sekta ya michezo katika shule 56 zilizopo katika mpango huo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Elimu Shule za Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Margareth Kapolesya, ambapo alisema kwa upande wa halmashauri yake, ina mpango wa kuboresha miundombinu yao yote ya michezo na si viwanja vya mpira wa wavu (valleyball) pekee.

**"Mpango huo ulitokana na uamuzi wetu wa kuiteua Shule ya Sekondari ya Unyahati kuwa ni shule ya mchepuo wa michezo, hivyo ikawa ni miongoni mwa shule 56 za mchepuo wa michezo nchini," alisema**

Kwa mujibu wa ofisa huyo mwenye dhamana ya kusimamia elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 shule hizo za mchepuo wa michezo nchini, ziliahidiwa kila moja kupewa shilingi milioni tano, lakini mpaka sasa bado hawajapokea kiasi chochote cha fedha hizo.

"Shule hizo za mchepuo wa michezo nchini katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, ziliahidiwa kupatiwa kila shule shilingi milioni tano, lakini mpaka sasa hatujapokea fedha hizo ingawa katika taarifa ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, wakati wa kufunga michezo ya UMISSETA mwaka 2024 pale mkoani Tabora alisema kuwa tayari shule 28 kati ya 56 zimetumiwa fedha hizo,"alibainisha.

# Dilunga 'alimisi vibe' la mashabiki Simba

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA na kiungo mshambuliaji wa zamani wa Simba, Hassan Dilunga, amesema kitu ambacho ana 'kimisi' kwa sasa ni shangwe la mashabiki wa timu hiyo wanapokuwa kwenye majukwaa ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye michezo ya kimataifa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, juu ya maisha yake binafsi na ya soka, Dilunga ambaye mashabiki wa Simba walimpa jina la HD, alisema hatoweza kuwasahau mashabiki wa klabu hiyo, si kwenye 'vibe' la kushangilia bali pia walipomsapoti wakati akiwa majeruhi na kufiwa na mtoto wake.

"Mashabiki wote wa Simba wapo moyoni mwangu, wajue hilo, nawapenda sana, unajua wakati napata majeraha ndiyo nilipata msiba wa mtoto wangu, walikuwa mstari wa mbele sana, wakanisaidia kwa hali na mali, sina cha kuwalipa, Mungu ndiye atawalipa, hilo ni suala langu binafsi, kwenye soka lile shangwe lao kule jukwaani hasa kwenye mechi za kimataifa 'nimelimisi', sana," alisema Dilunga.

Mchezaji huyo, atakumbukwa zaidi na wanachama na mashabiki wa Simba kwa krosi pasi yake kwa Clatous Chama, iliyozaa bao la tatu dhidi ya Nkana FC ya Zambia, Uwanja wa Benjamin Mkapa, uliochezwa, Desemba 23, 2018 na kuifanya Simba kushinda mabao 3-1, na kufanikiwa kutinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza tangu 2003.

Huo ukiwa ni mwanzo wa safari ya timu hiyo kucheza robo fainali sita ya michuano ya kimataifa kwa misimu saba. Hata hivyo, alisema kwa sasa anapenda kucheza michezo ya kimataifa akiwa na timu yake ya JKT Tanzania.

"Nimemisi sana kucheza mechi za kimataifa, si kidogo, kwa sababu najua ukubwa wa mashindano yake, furaha inayopatikana kwa mashabiki na wachezaji, natamani nicheze, lakini safari hii nikiwa na timu yangu ya JKT Tanzania, ili hawa vijana walio hapa wapate nafasi ya kucheza na waone thamani ya michuano hiyo," alisema.

Dilunga alimzungumzia mchezaji mwenzake wa JKT Tanzania, Said Ndemla, kuwa ni zaidi ya rafiki kwani alimpokea wakati anaingia kwenye Klabu ya Simba, naye akampokea kwenye klabu hiyo wanayochezea sasa.

"Tulikuwa tunafahamiana kabla, yeye alikuwa Simba mimi Mtibwa Sugar, nilipotaka kwenda Msimbazi yeye ndiye alinishawishi, na kunipokea akawa mwenyeji wangu.

"Yeye alianza kuondoka alienda Singida Big Stars, mwaka mmoja baadaye na mimi nikaondoka nikaja JKT Tanzania, na mimi nikampokea alipokuja hapa," alisema.

Dilunga aliichezea Simba kuanzia 2018 hadi 2023, ambapo kabla ya hapo alishawahi kuzichezea JKT Ruvu, Mtibwa Sugar na Yanga.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CUNHA AWA LULU

KLABU ya Aston Villa imejiunga na mbio za kumsaka mshambuliaji wa Wolves na Brazil, Matheus Cunha mwenye umri wa miaka 25, ambaye pia anazivutia Nottingham Forest, Chelsea, Arsenal, Tottenham na Manchester United. (***Barua***)

### RASHFORD MAMBO MAGUMU

JARIBIO la Barcelona kumsajili fowadi wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, huenda likashindikana kwa kuwa hawajauza wachezaji wa kutosha ili kupata fedha. (***ESPN***)

### DORGU OFA YA PILI

KLABU ya Manchester United itatoa ofa ya pili kwa Lecce kwa ajili ya kumnunua beki wa Denmark, Patrick Dorgu mwenye umri wa miaka 20, baada ya dau lao la pauni milioni 25 kukataliwa. ***(Fabrizio Romano)***

### AMORIM ASIKITISHWA USAJILI

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amesikitishwa na klabu hiyo kwa kutokuwanunua wachezaji wapya mwezi huu. (***Manchester Evening***)

### DURAN KUPEWA OFA

KLABU ya Saudi Arabia, Al-Nassr, inatayarisha ofa rasmi kwa ajili ya mshambuliaji wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 21. (***Telegraph***)

### BROBBEY MKATABA WA KUDUMU

WEST Ham imeambiwa itahitaji kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Brian Brobbey mwenye umri wa miaka 22, kwa mkataba wa kudumu kwani Ajax hawana nia ya kumtoa kwa mkopo. (***Fabrizio Romano***)

### REAL MADRID NA KIMMICH

REAL Madrid imeanza mazungumzo ya mapema na kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 29, kuhusu uhamisho wake, mkataba wake utakapomalizika. ***(Bild)***

### GARNACHO KUTUA CHELSEA

MCHEZAJI wa Manchester United, Alejandro Garnacho, atajiunga na Chelsea mwezi huu baada ya mazungumzo ya winga huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 20, kuhusu kuhamia Napoli kukwama. (***TeamTalks***)

### BROJA KUBADILISHWA

KLABU ya Everton inatumaini kumtumia mshambuliaji wa Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 23, kurudi Chelsea ili kubadilishana na viungo wa kati, Kiernan Dewsbury-Hall mwenye miaka 26 na Carney Chukwuemeka, 21. (***Guardian***)

### ZINCHENKO HANA OFA

ARSENAL haijapokea ofa yoyote ya kumnunua Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 28, licha ya kwamba mchezaji huyo anauzwa. (***Sky Sports***)

### FERGUSON AWINDWA

KLABU ya Brighton inafikiria iwapo itamruhusu mshambuliaji wake, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 20, kuondoka kwa mkopo mwezi huu huku kukiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazomtaka mchezaji huyo wa Kimataifa wa Jamhuri ya Ireland. (***Mail***)




# NEYMAR SAFARI KUREJEA SANTOS YAKARIBIA KUIVA

**JEDDAH,** Saudi Arabia

## Mkataba wake na Al Hilal kusitishwa, pande hizo mbili zinatarajiwa kukutana mapema wiki hii kwa...

NYOTA wa Brazil, Neymar, anakaribia kurejea katika klabu yake ya zamani ya Santos, kwa mujibu wa ESPN.

Neymar amebaki kwenye orodha ya Klabu ya Al Hilal ya Saudi Arabia, lakini kocha wa timu hiyo, Jorge Jesus, alisema mapema Januari kwamba mshambuliaji huyo "hawezi tena kucheza kwa kiwango tulichozoea", na hakusajiliwa kucheza Ligi Kuu ya Saudia na kumwacha akistahili kucheza Ligi ya Mabingwa wa Asia pekee.

Kutokana na hali hiyo, Neymar amekuwa akitafuta nafasi yake nyingine ya kucheza, na anaonekana kuipata kwenye klabu ambayo alianza nayo kucheza soka la kulipwa.

Vyanzo vya habari vinaiambia ESPN kwamba mkataba wa Neymar na Al Hilal huenda ukasitishwa, lakini maelezo ya mwisho bado yanajadiliwa.

Pande hizo mbili zinatarajiwa kukutana mapema wiki hii kwa matumaini ya kufikia makubaliano. Iwapo hilo litatokea, Neymar anatazamiwa kusaini mkataba wa miezi sita, ambao utakuwa na chaguo la kuongezwa mwaka mmoja zaidi.

Iwapo mkataba na Santos utakamilika, Neymar anatazamiwa kusafiri hadi Brazil wiki hii, na anaweza kuichezea Santos kuanzia Februari 5, mwaka huu.

Kwa kusitisha mkataba wake na Al Hilal, ambao ulitakiwa kumalizika msimu huu wa majira ya joto, Neymar angeachana na takriban dola milioni 65.

Hata hivyo, ESPN Brazil inaripoti kwamba Neymar bado amedhamiria kurejesha fedha kutoka kwa Al Hilal na kwamba mpango wowote unaohusisha hisa kwa Santos utakuwa mgumu sana kutekeleza kwa muda mfupi.

Kwa hivyo, ingawa mfumo wa kurejea kwa Santos upo kwa kanuni, bado kuna pointi za kushikamana.

Iwapo kurejea kwake Santos kutakamilika, itahitimisha sakata la uhamisho lililojumuisha uwezekano wa Neymar kutimkia Chicago Fire FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Marekani, MLS.

Hata hivyo, upendeleo wa Neymar ulikuwa kurudi Brazil ili kurejesha kiwango chake na ikiwezekana kurudisha nafasi yake timu ya taifa.

Neymar mwenye umri wa miaka 32, alivumilia kipindi kigumu akiwa na Al Hilal baada ya kujiunga na klabu hiyo ya Saudi Arabia kutoka Paris Saint-Germain msimu wa majira ya joto wa 2023 kwa ada ya dola milioni 97.6.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona, alipasuka mshipa kwenye goti lake la kushoto akiwa kwenye majukumu ya kimataifa muda mfupi baada ya kujiunga na Al Hilal.

Alirejea uwanjani Oktoba mwaka jana, lakini jeraha la misuli ya paja lilimfanya ashindwe kutoa mchango zaidi.

Alicheza mechi saba tu za ligi na mataji akiwa na bao moja pekee katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa ya Asia dhidi ya Nassaji Mazandaran mnamo Oktoba 3, 2023.

Licha ya misukosuko yake nchini Saudi Arabia, Neymar anabakia kuwa mmoja wa wachezaji wenye majina makubwa katika mchezo huo kutokana na uchezaji wake pamoja na Lionel Messi na Luis Suarez wakati akiwa na Barcelona kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.

Wakati huo, alikuwa sehemu ya timu zilizoshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji mawili ya LaLiga, na matatu ya Copa del Reys.

Baadaye alihamia PSG mwaka 2017 na kushinda mataji matano ya Ligue 1, matatu ya Coupe de Frances na mawili ya Coupe de la Ligues.

Neymar alianza soka lake la kulipwa akiwa na Santos mwaka wa 2009, na kuwaongoza kutwaa ubingwa wa Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini) mwaka 2011, alipofunga katika mechi ya mkondo wa pili wa fainali ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Peñarol.

Katika ngazi ya kimataifa, Neymar ameichezea Brazil mara 128, akifunga mabao 79.

Alikuwa sehemu ya timu ya Brazil iliyoshinda medali ya dhahabu kwenye Olimpiki ya majira ya joto ya 2016, ambayo Brazil ilikuwa mwenyeji.



# AMORIM AMCHOKA MAZIMA RASHFORD

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim, amesema afadhali kumchezesha kocha wake wa makipa, Jorge Vital mwenye umri wa miaka 63, katika timu yake kuliko Marcus Rashford, isipokuwa kama fowadi huyo atajituma kwenye mazoezi.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa England, Rashford aliachwa nje ya timu kwa mchezo wa 11 mfululizo na Amorim, wakati United iliposhinda bao 1-0 kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Fulham Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alisema mwezi uliopita kwamba yuko tayari kutafuta "changamoto mpya" nje ya Old Trafford baada ya kuachwa katika ushindi wa United wa mabao 2-1 dhidi ya Manchester City kwenye Uwanja wa Etihad Desemba 15, mwaka jana, lakini Rashford hadi sasa hajawezi kupata klabu mpya wakati wa dirisha hili la uhamisho la Januari.

Na licha ya washambuliaji Rasmus Hojlund na Joshua Zirkzee kufunga bao moja pekee kati yao tangu mwanzoni mwa Desemba, Amorim alisema hatamrejesha Rashford kwenye timu isipokuwa kama atabadilisha mtazamo wake.

"Ni sawa, daima ni sababu sawa," alisema Amorim alipoulizwa kwa nini aliendelea kutomtazama Rashford.

"Sababu ni mazoezi, jinsi ninavyoona wanasoka wanapaswa kufanya mazoezini, maishani, ni kila siku, kila undani.

"Kwa hiyo mambo yasipobadilika sitabadilika, ni hali sawa kwa kila mchezaji. Ukifanya kiwango cha juu, ukifanya mambo sahihi tunaweza kumtumia kila mchezaji. Na unaweza kuona leo kwenye benchi, tunakosa kasi kidogo ya kwenda na kubadilisha mchezo."

Amorim, ambaye aliwasili kutoka kwa mabingwa wa Ureno Sporting CP mnamo Novemba mwaka jana, jana Jumatatu alisherehekea siku yake ya kuzaliwa kwa kutimiza umri wa miaka 40.

Lakini baada ya ushindi wa Fulham, alisema anahisi mzee zaidi baada ya kukaa kwa muda mfupi United.

"Si 40 ... mimi nina 50!" alisema kwa kutania. "Baada ya miezi miwili nikiwa Manchester United, ni miaka 50. Ni bahati nzuri kutumia siku yangu ya kuzaliwa ya kutimiza umri wa miaka 40."

# Flick akunwa njaa ya mabao ya Barcelona



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, amesifu njaa ya mabao ya timu yake walipoizaba Valencia 7-1 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Jumapili.

Fermin Lopez alifunga mara mbili, huku Frenkie de Jong, Raphinha, Ferran Torres na Robert Lewandowski, pia wakifunga, hivyo Barca kukifikisha mabao 101 katika mashindano yote msimu huu.

Ilikuwa ni mara ya pili kwa Barca kufunga mabao saba katika mchezo mmoja chini ya Flick, huku sasa wakiwa wamefunga mara nne au zaidi katika mechi 14 kati ya 32 katika kampeni hii.

"Ninapenda njaa hii ambayo timu inayo, ambayo inaonekana kwenye mechi, haswa leo (juzi)," alisema Flick katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo.

"Haijakamilika na 2-0 au 3-0. Wanaenda hadi mwisho wa mechi. Hiki ndicho ninachopenda na tunachopenda kucheza. Ni vizuri kuona hili."

Barca waliwapeperusha Valencia kwa mabao matano katika kipindi cha kwanza. De Jong, Torres na Raphinha wote walifunga ndani ya dakika 15, huku Lopez akiongeza mengine mawili kabla ya mapumziko.

Ushindi huo unaifanya Barca kusalia na pointi tatu nyuma ya Atletico Madrid iliyo nafasi ya pili, lakini bado wamepitwa pointi saba na vinara, Real Madrid.

Flick pia alionekana kupendekeza Wojciech Szczęsny kubakia kama kipa chaguo la kwanza kwa siku za usoni, mbele ya Iñaki Peña, baada ya kumpatia mechi yake ya kwanza ya LaLiga dhidi ya Valencia.

Barca wanataucheza tena kesho Jumatano watakapowakaribisha Atalanta katika mchezo wao wa mwisho wa awamu ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa tayari wamejikatia tiketi ya kutinga hatua ya 16-bora.

# Postecoglou: Siijui kesho yangu Spurs

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, amekiri kwamba kibarua chake si salama baada ya timu hiyo kufungwa kwa mara ya 13 katika Ligi Kuu ya England, msimu huu dhidi ya Leicester City Jumapili.



Spurs walichukua uongozi kupitia kwa Richarlison katika kipindi cha kwanza, huku mabao ya Leicester City yakifungwa na Jamie Vardy na Bilal El Khannouss.

Kikosi cha Ruud van Nistelrooy, ambacho kilikuwa kimepoteza michezo saba ya awali ya ligi, kilijiweka sawa kwa kipindi kizima cha mechi hiyo ili kupata pointi tatu ambazo ziliwaondoa kwenye eneo la kushushwa daraja na kuzidisha shinikizo kwa kocha wa Spurs raia wa Australia.

Alipoulizwa kama anafaa kubaki kwenye kiti hicho, Postecoglou alisema: "Nani anajua?.

"Unapokuwa kocha wa klabu ya soka, unaweza kuhisi kuwa katika mazingira magumu na kutengwa, sihisi hivyo. Wachezaji wanatoa kila kitu. Ninazingatia hilo na kujaribu kusaidia wachezaji."

Kocha huyo wa zamani wa Celtic aliongeza kuwa, kushindwa kwake ni chungu, ingawa hataki kuwaonesha wakosoaji kwamba mbinu zake hazifanya kazi.

"Ndio inauma, inauma sana, wachezaji walitoa kila kitu tena, tutaangalia mambo mengi, lakini katika suala la juhudi siwezi kuuliza zaidi ya kundi hili, mambo hayakwenda njia yetu leo," alisema Postecoglou.

"Haiingii akilini kujaribu kuwashawishi watu, nimekuwapo kwa muda wa kutosha kwamba watu watahukumu tulipo kwa sasa, ambayo haijakuwa nzuri vya kutosha.

"Katika siku 10 zijazo tunapaswa kuwarejesha baadhi ya wachezaji wa maana ambao watasaidia. Bado tuna fursa nzuri za kufanya matokeo (kupatikana) - nina uhakika hilo litafanyika."

# HABARI MICHEZO

## Fadlu na hesabu kali za kuiliza Tabora Utd

INATOKA UKURASA 24

wadogo hawana ukomavu, kwa mechi hii tumejifunza, na hili ndilo tulikuwa tunahitaji, kama wameweza kupambana na Simba na kupelekeshwa kwa kasi ile, nadhani watakuwa wamekomaa na kujifunza kwani hakuna timu yoyote ya levo yetu inayoweza kucheza kama hivi, ila na sisi tutakwenda kuzipelekesha kama Simba ilivyotufanyia," alisema.

Mabao ya Simba yalifungwa na Velentino Mashaka, Ladack Chasambi, Joshua Mutale, Steven Mukwala, Edwin Balua na moja la kujifunga wenyewe kupitia kwa Patrick Sebastian.

## Ramovic amvulia kofia Mwenda

INATOKA UKURASA 24

yetu."

Akizungumza baada ya kucheza mchezo wake wa kwanza akiwa na Yanga, Mwenda, alifurahi kuwa na mwanzo mzuri kwani si wachezaji wote wanaokwenda timu mpya na kufanya vizuri.

"Niwapongeze wachezaji wenzangu, ushirikiano ulikuwa muhimu katika mchezo wa kwanza, unajua ndiyo kwanza nimefika, lakini mwanzo nilioanza nao ni mzuri sana.

"Nilikuwa na hamu sana ya kupata nafasi, na nilipoipata nikasema leo ngoja niitumie ili watu wajue kuwa kuna mchezaji mpya amejiunga, unaposajiliwa kipindi cha dirisha dogo, hutakiwi kupewa muda, unaingia moja kwa moja kuisaidia timu," alisema Mwenda ambaye kabla ya kuwa Singida Black Stars, aliichezea Simba.



Mchezaji huyo alitoa 'asisti' mbili kwenye bao la Prince Dube, dakika ya 66, likiwa bao la pili kwenye mchezo huo na la tano dakika ya 84, lililounganishwa kwa kichwa na Mudathir Yahaya.

"Katika 'asisti' hizo nimependa ile ya pili, maana Kibwana Shomari aliniwekea kwenye njia kwa wakati sahihi na mimi nilikuwa kwenye mwendo, nilichofanya nikapiga krosi iliyokuwa na malengo mawili, ikimkuta mtu afunge au wao wajifunge wenyewe kwenye harakati za kuokoa," alisema Mwenda.

Yanga iliongeza wachezaji wawili tu kipindi cha dirisha dogo la usajili, ambapo mbali na Mwenda, yumo pia, Jonathan Ikangalombo, winga aliyesajiliwa kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ambaye hakucheza mechi hiyo, na kwa mujibu wa kocha Ramovic, alikuwa mgonjwa.

# WACHEZAJI KILIMANJARO WONDERS WAFURAHIA KUONEKANA KWENYE TV

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Kilimanjaro Wonders, wamesema pamoja na kufungwa mabao 6-0 dhidi ya Simba, kwenye mchezo wa Kombe la FA katika Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi, lakini wamefurahia kuonekana kwenye televisheni nchi nzima, huku wakidai ilikuwa ni moja ya malengo yao ili kuwaonesha watu kuwa wana vipaji vya kusakata kabumbu.

Wachezaji hao, Hamisi Ramadhani, Faraji Rashid, Patrick Sebastin na Khatibu Kigasa, walisema kitendo cha kupangiwa kucheza na Simba, walijua ni fursa ya kwenda kuonesha watu kuna vipaji vilivyojificha, na kwamba licha ya kufungwa mabao hayo, wameonesha vipaji vyao na wengi wamefurahi.

Faraji, ambaye mashabiki wa soka wamempachika jina la 'Salah', wakimfananisha na mchezaji wa Livepool ya England, Mohamed Salah, amesema amefurahi kuona mashabiki wengi na hata wachezaji wa Simba wamefurahishwa na kiwango chake.

"Nilikuwa nacheza huku nikijua tunaoneshwa kwenye TV, kwa hiyo nilikuwa nafanya vitu ambavyo watu wataviona, nilitaka watu waone kipaji changu ili nionekane, nichukuliwe na mimi niweze kwenda kwenye timu zenye uwezo nipate kipato cha kuniwezesha maisha yangu kuwa mazuri," alisema winga huyo machachari.

Alisema awali alikuwa na wasiwasi kucheza na wachezaji wakubwa kwani ni mara yake ya kwanza kuwaona laivu

"Kitu kipya nilichokutana nacho uwanjani ni presha ya mashabiki, kupokea pasi mbele ya mchezaji mkubwa ambaye huwa unamuona kwenye TV, nayo pia ilikuwa kama nina kigugumizi hivi, lakini baadaye nikazoea," alisema.

Hamisi, alisema alikuwa anacheza ili aonekane kwenye televisheni akionesha uwezo wake, kwani lengo lake anatakamni kucheza kwenye Kituo cha TFF.

"Ndoto yangu kubwa ni kupambania nembo ya timu ya taifa, ukiangalia wana michuano ya CHAN Agosti na AFCON 2027, natamani niwe mmoja wa wachezaji hao, pia kuichezea Simba kwenye Ligi Kuu misimu kadhaa ijayo," alisema mchezaji huyo aliyecheza beki wa kati.

GOFU...




Washindi wa Mashindano ya Gofu ya KCB Lugalo New Year Competition, wakiwa pamoja na viongozi wa Benki ya KCB Tanzania, baada ya kukabidhiwa zawadi, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Kissu apania kuirejesha Polisi Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya Polisi Tanzania kutangaza kumsajili kipa mkongwe, David Kissu Mapigano, mwenyewe amefunguka kuwa ameletwa kwenye kikosi hicho kwa lengo la kusaidiana na wenzake kuhakikisha timu hiyo inarejea Ligi Kuu.

Kissu, ambaye amewahi kuidakia, Biashara United wakati iko Ligi Kuu Tanzania Bara, alisema Polisi Tanzania ni timu kubwa, hivyo ni heshima kubwa kwake kusajiliwa na timu hiyo, akisema kutokana na hilo anataka kuipeleka kwenye hadhi yake inayotakiwa.

"Nimekubali kujiunga na Polisi Tanzania iliyo Ligi ya Championship, kwa sababu ni timu kubwa, kila mtu anaifahamu, imeshacheza Ligi Kuu na ina hadhi hiyo, ni bahati mbaya tu ipo huku, kwa hiyo nilipopata nafasi hiyo sikuikataa, lengo kuwa hapa ni kushirikiana na wenzangu, viongozi na benchi la ufundi kuirudisha huko juu, mimi binafsi nitatumia uzoefu wangu wote kufanikisha ushindi, unajua mpira wa miguu unaanzia langoni, kukiwa na kipa ambaye ni bora na mzoefu, timu inakuwa ipo salama zaidi, mengine yanafuatia.

"Najua Ligi ya Championship ni ngumu hasa michezo hii ya mzunguko wa pili, ila naamini tukishirikiana tutafanikiwa," alisema kipa huyo.

Kissu akiongea hayo, timu yake juzi hiyo hiyo, ilipokea kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Mbuni FC, mechi iliyochezwa, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha. Mabao ya washindi yalifungwa na Malulu Thomas dakika ya 33 na Rishedy Hassan dakika ya 44.

Kipigo hicho kinaifanya Polisi Tanzania, iliyoshuka daraja msimu wa 2022/23, kukamata nafasi ya 10 ya msimamo wa ligi ikiwa na pointi 19, huku washindi wa mchezo huo, Mbuni wakipanda hadi nafasi ya tisa ikifikisha pointi 23, timu zote zikicheza michezo 16.

# Michezo

Jumanne Januari 28, 2025

Nipashe




Amorim amchoka mazima Rashford UKURASA 22

# Fadlu na hesabu kali za kuiliza Tabora Utd

● ● ● Aeleza namna alivyoivaa Kilimanjaro Wonders akichanga karata kwa 'Nyuki' hao, pia atoa sababu ya...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema alikuwa uwanjani kuiongoza timu yake ikicheza mechi ya Kombe la FA dhidi ya Kilimanjaro Wonders, lakini akili yote ikiwaza mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Tabora United, utakaopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Akizungumza juzi baada ya timu yake kuibugiza Kilimanjaro Wonders mabao 6-0 na kusonga mbele kwenye hatua inayofuata ya michuano ya FA, Fadlu, alisema aliutumia mchezo huo ili kuwapa nafasi wachezaji wake wote ambao hawapati muda wa kucheza kwenye Ligi Kuu, kupata dakika za kucheza, wakati huo huo akiweka sawa silaha zake anazozitegemea kwenye mchezo unaofuata.

"Ilikuwa ni mechi muhimu kwa wachezaji wote kupata muda wa kucheza, hasa ambao hawakuwa wanapata nafasi, ni kweli kuna baadhi ya wachezaji hawakuwapo, Aishi Manula amepatwa na mafua, wengine walikuwapo, lakini ilibidi niwapumzishe kwa sababu tuna mchezo mgumu dhidi ya Tabora United," alisema Fadlu.

Alisema hata mchezo huo ulikuwa ni kama sehemu tu ya maandalizi ili kuangalia baadhi ya wachezaji ambao wamekuwa hawaanzi mara kwa mara kuwatumia kuongeza nguvu kwenye mechi hiyo pindi itakapohitajika.

"Tumeutumia kama mazoezi, tunaangalia wachezaji ambao wamekuwa na viwango vya kutosha kuweza kuongeza nguvu katika mchezo wetu huo muhimu wa Ligi Kuu, pale wanapohitajika kuingia uwanjani kwenda kufanya kile ambacho tumewatuma," alisema Fadlu, raia wa Afrika Kusini.

Akiuzungumzia mchezo huo, alisema wamecheza na timu ambayo kiwango chao ni tofauti kabisa na cha Simba, ila baadhi yao wana vipaji.

**"Vijana hawa wa Kilimanjaro Wonders ni wachanga, walijitahidi kwa kadri ya uwezo wao, lakini viwango vya timu na vya mchezaji mmoja mmoja vilikuwa tofauti kabisa, ila nimeona baadhi wana vipaji," alisema.**

Kocha Msaidizi wa timu ya Kilimanjaro Wonders, Wilbard Pacho, alisema lengo lao kubwa lilikuwa ni kupata angalau bao moja la kufutia machozi, lakini kwa bahati mbaya walilikosa.

"Tuliangalia ubora na udhaifu wa Simba, lakini tulikuja hapa angalau tupate bao moja au mawili, watufunge lakini mabao 3-1, 5-2, hatukutaka tutoke uwanjani bila bao la kufutia machozi, lakini ubora wa wachezaji wa Simba umetuadhibu," alisema.

Hata hivyo, alisema wamepata nafasi ya kujifunza, na hilo litawasaidia kwenye mechi zao watakazocheza.

"Wachezaji wetu ni vijana

INAENDELEA UK. 23



Fadlu Davids

# Ramovic amvulia kofia Mwenda

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesifu kiwango kilichooneshwa na beki mpya wa kushoto wa Yanga, Israel Mwenda, kwenye mchezo wa Kombe la FA, uliopigwa, Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam dhidi ya Copco FC, akisema ujio wake na kile alichoonesha, kitaongeza nguvu kwenye timu kufikia malengo waliyojiwekea.

Ramovic alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana, siku mbili baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Copco FC.

Katika mchezo huo, Mwenda, alicheza mechi yake ya kwanza tangu asajiliwe kutoka Singida Black Stars, huku akitoa pasi za mwisho mbili, akichangia ushindi wa idadi hiyo ya mabao dhidi ya timu hiyo yenye maskani yake jijini Mwanza.

"Huwa napenda kuzungumza habari ya timu kwa ujumla kila mara, kwa sababu wote sisi ni wamoja, tunafanya kazi pamoja, hatushindi mechi kwa mchezaji mmoja mmoja, bali timu.

"Kwa maana hiyo siwezi kusema mchezaji fulani amecheza vizuri zaidi na mwingine hajacheza vema, siwezi kuwatoa kasoro wachezaji wangu kwani tukishinda tunashinda pamoja na tukifungwa tunapoteza wote," alisema Ramovic na kuongeza:

"Nikirudi kumzungumzia Mwenda, ni kwamba anaonekana yupo vizuri, amefanya vema kwenye mchezo wetu, na hiki kwake ni kitu muhimu ili kutupa imani, anaonekana atatuongezea kitu kuelekea kwenye malengo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >